# Nipashe

Alhamisi Desemba 24, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580439

The Guardian digital

ww...com

nipash...eTZ

nipasheTZ

0745 700710




ama

ALHAMISI DESEMBA 24, 2020 AFYA NA MAZINGIRA

Maisha ya ngono na mimba za ajabu visiwa vya Mwanza Ukurasa 12

Operesheni tohara inavyosambaratisha Ukimwi ulioshika kasi mkoa Shinyanga Ukurasa 13

Mamlaka za Maji zamudu kusambaza, ila mijini yanayopotea njiani tishio Ukurasa 14

## Namna ilivyo tatizo la mama anapokosa hedhi kwa wakati

Na Jackson Paulo

HALI ya kukosa hedhi kitaalamu inaitwa 'Amenorrhea'. Hiyo inahesabika pale mwanamke anapokosa walau vipindi vitatu mfululizo vya hedhi au binti hajaanza, angalau tayari ana umri wa miaka 15.

Kwa kawaida hedhi huwa mara moja kila mwezi, sababu ya kawaida inayochangia kukosekana hedhi ni ujauzito. Dalili kuu ya shida hiyo ni pamoja na mtu kupata dalili nyinginezo zinazoambatana na kukosa vipindi vya hedhi, ambazo ni pamoja na; utoaji maziwa kwenye chuchu, maumivu ya kichwa, kupoteza kuona vizuri, maumivu ya nyonga, na kutokwa chunusi.

Zipo sababu nyingine zinazochangia kuwa, ni pamoja na tatizo katika mfumo wa uzazi au katika tezi zinazosaidia kudhibiti viwango vya homoni mwilini.

Mwanamke akiwa amelala, akisumbuliwa na tumbo. PICHA: MTANDAO.

### UNAMUONAJE DAKTARI?

Mgonjwa anaweza kumuona daktari, kama hajapata angalau vipindi vitatu mfululizo vya hedhi au hajawahi kupata hedhi na tayari umeshafikisha umri wa miaka 15.

Kukosa hedhi kunaweza kuchangiwa na sababu mbalimbali. Baadhi ni za kawaida katika maisha ya mwanamke na kuna wakati inaweza kuwa ni kutokana na athari ya dawa au kiashiria cha tatizo jingine la kiafya. Hapo, sababu zinazochagia kukosekana hedhi na kuna sababu kadhaa.

Mwanzo, unaanzia katika maisha ya kawaida ya mama, zipo sababu za asili na kawaida zaidi, zinamfanya akose hedhi. Ni pamoja na ujauzito wa mwili, kunyonyesha na ukomo wa hedhi wa asili uitwao kitaalamu 'menopause'.

Pia, katika matazamo wa uzazi wa mpango matumizi ya dawa za uzazi zinaweza kuchangia kukosekana hedhi kwa baadhi ya wanawake.

Hata baada ya kusitisha matumizi ya dawa hizo, bado kuna uwezekano wa kuchukua muda kidogo kwa mzunguko wa hedhi kurejea katika hali ya kawaida.

Tatu, ni matumizi ya baadhi ya dawa zinazomsababisha mwanamke akose vipindi vya hedhi. Kuna baadhi ya dawa zinafanya hedhi kuwa tatizo.

Kuna dawa za magonjwa ya akili, matibabu ya saratani (chemotherapy), dawa za kuzuia mfadhaiko (antidepresants), dawa za kutibu shinikizo la damu, pia za mzio 'allergy'.

Nne, kuna suala la mtindo binafsi wa maisha, kuna wakati humchangia mtu kupata tatizo la hedhi, mathalan uzito wa mwili ulio mdogo kupitiliza huathiri ufanyaji kazi wa homoni, hivyo kusababisha kushindwa kuachiliwa kwa 'yai' kutoka kwenye ovari.

Ni hali ambayo kitalaamu inawafanya kinamama kutopata hedhi. Kinamama ambao wana tatizo la kula, hushindwa kupata vipindi vya hedhi, kwa sababu ya mabadiliko ya homoni yasiyo ya kawaida.

Pia, kuna ufanyaji mazoezi uliopitiliza kwa wanawake wanaoshiriki mafunzo na uwezekano mwingine uko katika msongo wa mawazo, unaoleta mabadiliko kwenye sehemu ya ubongo.

Hata hivyo, vipindi vya kawaida vya hedhi huanza kurejea tena kadri msongo huo unavyopungua.

Lingine ni kuwapo uwiano usio sawa mwilini na unapaswa kuwapo. Ikiwa mwili una tatizo, ni hali inayoweza kuchangia kukosekana hedhi kwa mwanamke. Uwiano wa homoni mwilini unasimamiwa na mengi, ikiwa ni pamoja na kuathirika kwa ufanyaji kazi wa tezi ya kooni na ukomaji mapema wa hedhi ya asili.

Eneo lingine lenye mchango wa athari ni maumbile ya viungo vya uzazi, ambavyo kuna wakati vinachangia mtu kutopata hedhi. Hapo inajumuisha kuwapo kovu katika mji wa kinababa na mwanamama.

Ni hali inayotokea, kuegemea sababu kadhaa kama vile operesheni wakati wa kujifungua (cesarean section) na matibabu ya tatizo la uvimbe kwenye mji wa mimba.

Pia, inawezekana mwanamke anatokea kukosa viungo vya uzazi. Mwanamama anaweza akazaliwa na tatizo la kukosa mfumo wa uzazi kama vile mji wa mimba, kizazi au uke. Iwapo mfumo wa uzazi haupo, ni kawaida hali hiyo kumtokea.

Kunaweza kuwapo nyama nyepesi sehemu ya uke, inayozuia utokaji damu kutoka kwenye mji wa uzazi kuelekea nje.

### HATARI & MADHARA

Hapo inaingia historia ya familia yake, iwapo kuna watangulizi walishapata tatizo la kukosa hedhi, nawanamrithisha.

Tatizo la mlo; ikijumuisha ulafi kupita kiasi au kinyume chake, kula kidogo na kufanya mazoezi magumu. Madhara yanayoweza kuikabili muathirika huyo ni matatizo ya ugumba, kwani mama asiyepata hedhi, hapati ujauzito.


Pia, kuna hatari kiafya ya udhaifu wa mifupa, inayotokana na kiwango kidogo cha homoni aina ya estrojeni, inayosababisha kudhoofika mifupa.

• *Baruapepe: jacpole@gmail.com*

UKURASA 11

**'DAY CARE'** nyingi Dar hatarishi kwa usalama wa watoto

UKURASA 3



**DK. MPANGO** ataka mashirika kujieleza kwa mapato kiduchu

UKURASA 3

# Ajali za bodaboda zinavyoangamiza maelfu Watanzania

UKURASA 2



Moja ya ajali za waendesha pikipiki zilizotokea jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

## Trafiki Dar wakusanya faini bil. 17/- miezi 11

UKURASA 2

## Mbaroni tuhuma kumpiga dereva lori

UKURASA 4

**MICHEZO** **MSHAMBULIAJI LUPOPO ASAJILIWA RASMI AZAM** UK. 23

**MAONI, KATUNI UK. 6**



Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya I & M, Baseer Mohammed (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Wateja wa Rejareja, Lilian Mtali (wa nne kulia) pamoja na baadhi ya wateja wa benki hiyo, wakizindua huduma mpya ya Rafiki ChatBanking ambayo inawawezesha wateja kupata huduma za kibenki kwa urahisi zaidi kwa njia ya WhatsApp kwenye simu ya mkononi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi Dar wakusanya bil. 17/- faini

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kupitia Kikosi chake cha Usalama Barabarani, limekusanya Sh. bilioni 17.2 katika kipindi cha miezi 11 iliyopita kutokana na faini za makosa ya barabarani.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu matukio yaliyojitokeza ndani ya kipindi hicho mkoani mwake.

Alibainisha kuwa katika kipindi hicho cha miezi 11 kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu, jumla ya ajali za barabarani 537 ziliripotiwa kulinganishwa na ajali 1,169 zilizoripotiwa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka jana, zikiwa zimepungua ajali 632.

"Ajali za vifo mwaka huu zilizotokea ni 58 wakati mwaka 2019 zilikuwa ni 77 ikiwa ni upungufu wa ajali 19, sawa na asilimia 25. Waliojeruhiwa kwa ajali mwaka huu ni 521 na waliofariki dunia kutokana na majeraha ya ajali ni 73.

"Mwaka jana katika kipindi kama hicho waliojeruhiwa walikuwa ni 1,072 ikiwa ni upungufu wa majeruhi 551, sawa na asilimia 51 na waliofariki dunia walikuwa 87, sawa na asilimia 16," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema kwa mwaka huu, jumla ya magari yaliyokamatwa yalikuwa ni 422,932, pikipiki 5,604, daladala 160,977, magari binafsi na malori 261,955 na bodaboda waliofikishwa mahakamani kwa makosa ya kutovaa kofia ngumu na kupakia mishikaki ni 142.

"Jumla ya makosa yaliyokamatwa ni 563,909, magari yaliyokamatwa kupita kwenye barabara za mwendokasi ni 176, waliofikishwa mahakamani ni 34, majalada yaliyoko kwa mwanasheria ni 54 na yaliyoko chini ya upelelezi ni 88," alisema.

Kamanda Mambosasa aliyataja baadhi ya matukio ya uhalifu yaliyotokea kuwa ni pamoja na lile la wizi wa fedha Sh. bilioni 1.2, Dola za Marekani 402,000 na Euro 27,700 za Benki ya NBC lililodaiwa kufanywa na waliokuwa wafanyakazi wa kampuni ya ulinzi G4S.

Alitaja tukio lingine ni la wizi wa fedha Sh. bilioni 2.08 za Benki ya NMB zilizodaiwa kuibwa na waliokuwa walinzi wa SGA, jumla ya watuhumiwa 32 walikamatwa wakituhumiwa kuhusika na wizi huo.

Alisema makosa ya jinai yaliyoripotiwa mwaka huu ni 128,064 wakati kwa mwaka jana yalikuwa ni 138,024, ikiwa ni sawa na upungufu wa makosa 9,960 (asilimia saba).

"Jumla ya matukio makubwa 9,915 yaliripotiwa katika vituo vya polisi wakati kipindi kama hicho mwaka 2019 yalikuwa 11,066 ikiwa ni upungufu wa matukio 1,151 (asilimia 10)," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema makosa ya wizi wa silaha yalikuwa mawili wakati mwaka jana yalikuwa manne, unyang'anyi wa kutumia silaha yalitokea 79 huku mwaka jana yalikuwa ni 82.

"Unyang'anyi wa kutumia nguvu yalitokea matukio 333 wakati mwaka jana yalikuwa 202, uvunjaji yalikuwa 3,600 na mwaka jana yalikuwa ni 3,624, wizi wa magari jumla ya matukio 126 wakati mwaka jana 69, wizi wa pikipiki matukio 1,450 wakati mwaka jana yalitokea 1,662, wizi wa mifugo matukio 79 wakati mwaka jana yalikuwa 88, mauaji yalitokea 218 wakati mwaka jana yalikuwa ni 155," alisema.

Alisema matukio ya ubakaji yalikuwa ni 1,004 wakati mwaka jana yalikuwa ni 820, kulawiti matukio 364 na mwaka jana yalitokea 293.

"Wizi wa watoto kulikuwa na matukio 10 wakati mwaka jana yalikuwa ni 20 ikiwa ni ongezeko la matukio 10," alisema.

Alisema waliwakamata watuhumiwa wa ujambazi sugu 333 waliodaiwa kujihusisha na makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha, unyang'anyi wa kutumia nguvu na wizi wa magari.

Kamanda Mambosasa alisema katika ukamataji huo, walipata silaha tisa na risasi 108.

FORM 84

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT DAR ES SALAAM
(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 71 OF 2020
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MOHAMMED NASSOR ALI AL-ALAWY
DECEASED
AND
IN THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY

1. FATMA ABDALLAH SALUM
2. NASSOR MOHAMMED NASSOR
3. ABDALLAHNASSOR ALLY
4. MUNDHIR MOHAMMED NASSOR

} ADMINISTRATORS AND ADMINISTRATRIX

**NOTICE TO CREDITORS**
**(Made under Rule 111 on the Probate and Administration of Estates Act, CAP 352 R.E. 2002)**

**NOTIC**E is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above-named **MOHAMMED NASSOR ALI AL-ALAWY** deceased, who died at TMJ Hospital in Dar es Salaam on the 04th day of August 2020 and probate of whose letters of administration of whose estate were granted to us **FATMA ABDALLAH SALUM, NASSOR MOHAMMED NASSOR, ABDALLAH NASSOR ALLY AND MUNDHIR MOHAMMED NASSOR** all residing at Plot No. 8/1 Oyster Bay, Tumbawe Street of P. O. Box 5424 Dar es Salaam, by the High Court of Tanzania at Dar es Salaam on the 14th day of December, 2020, before Honourable A. K. Rwizile, J. are hereby required to send their claim to us at the following address within two month from the date of publication of this notice at the expiration of which time we shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims of which we then shall have had notice.

**FATMA ABDALLAH SALUM**
**P. O. BOX 5424**
**DAR ES SALAAM**

**NASSOR MOHAMMED NASSOR**
**P. O. BOX 5424**
**DAR ES SALAAM**

**MUNDHIR MOHAMMED NASSOR**
**P. O. BOX 5424**
**DAR ES SALAAM**

**ABDALLAH NASSOR ALLY**
**P. O. BOX 5424**
**DAR ES SALAAM**

# Ajali za bodaboda zazidi kuwa tishio

**Na Christina Mwakangale**

AJALI za bodaboda zimeendelea kugharimu maisha ya watu baada ya taarifa kutoka Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) kuonyesha kuwa kwa mwaka 2008 hadi 2019, nusu ya majeruhi walitokana na vyombo hivyo vya usafiri. Katika kipindi hicho, majeruhi 110,679 walipokewa MOI kati yao majeruhi waliotokana na ajali za bodaboda ni 59,671, magari 21,711 na ajali zingine ni 29,297.

Joshua Ngahyoma, Ofisa Takwimu wa taasisi hiyo, aliiambia NIPASHE jana jijini Dar es Salaam alisema takwimu zinaonyesha waathirika wa ajali hizo ni pamoja na madereva, abiria na watembea kwa miguu. Ngahyoma alisema asilimia 70 ya wagonjwa wanaopokewa MOI kutokana na ajali hulazwa wodini, huku asilimia 10 hadi 15 wakifanyiwa uchunguzi.

"Makundi ya aina tatu kutokana na pikipiki, magari na ajali nyingine. Makundi ya ajali nyingine ni ambazo mtu alifika MOI kutokana na kuanguka, kipigo au walipigana, waliteleza," alisema Ngahyoma.

Alisema kuhusu takwimu za waliopokewa MOI, alisema mwaka 2018 ajali zilizosababishwa na bodaboda ziliwafikisha katika taasisi hiyo madereva majeruhi 1,863, wakiwamo abiria 1,154 na watembea kwa miguu 976, huku ajali zingine wakiwa 1,805.

Ofisa huyo aliongeza kuwa mwaka 2019 walipokewa madereva 2,920, abiria 1,607 na watembea kwa miguu 1,203 ambao chanzo cha ajali kikiwa ni bodaboda huku ajali zingine wakiwa 2,670. Pia alisema kipindi kama hicho cha mwaka 2018, ajali za gari zilisababisha madereva majeruhi 754, abiria 903 na watembea kwa miguu 829.

Ngahyoma alisema mwaka 2019 majeruhi wa ajali za gari walikuwa madereva 720, abiria 1,056 na watembea kwa miguu 768.

Katika taarifa iliyotolewa kwa waandishi wa habari wiki hii na Jeshi la Polisi na kuorodhesha matukio yaliyotikisa mwaka 2020 na kukabiliana nayo ni pamoja na ajali.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Libaratus Sabas, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, alisema ajali za barabarani zimepungua kwa mwaka huu.

Alisema mwaka jana kulitokea ajali za barabarani 2,722 na kusababisha vifo 1,117 na majeruhi 2,717, lakini kwa mwaka huu hadi Novemba, ajali zilikuwa 1,800 na waliofariki dunia 1,158 na majeruhi 2,089.

HABARI KITAIFA

# 'Day Care' nyingi Dar majanga

**Na Christina Mwakangale**

HALI ya vituo vya malezi kwa watoto, maarufu kama 'day care', vilivyoko kwenye maeneo tofauti ya makazi ya watu jijini Dar es Salaam, haviridhishi, huku Wilaya ya Ilala ikivifungia vituo 19.

Pia imebainika waanzishaji wa vituo hivyo, huvianzisha bila kufuata vigezo vilivyowekwa kwenye Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Manispaa ya Temeke, Theresia Nkwanga, aliyasema hayo hivi karibuni akizungumza katika kituo kimoja cha redio nchini kuhusu vituo hivyo.

Nkwanga alisema manispaa imekwishatoa tangazo kwa wananchi hasa wenye vituo hivyo na ambao hawajavisajili, wachukue uamuzi wa kuvifunga kabla ya sheria kuchukua mkondo wake.

"Adhabu ya sheria hiyo, vituo vikikiuka taratibu, mmiliki atatakiwa kulipia faini ya Sh. 100,000 kila siku, kwa kipindi ambacho alipewa tangazo la kufunga kituo na kukaidi."

Alisema kituo kinatakiwa kuwa na usalama wa kutosha, kuwapo kwa uzio, madirisha yenye kupitisha hewa na chumba kimoja kisizidi watoto 25.

Suzana Thomas, Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Ilala, alisema tayari wamevifungia vituo 19 kutokana na kukiuka utaratibu na kukutwa na makosa mbalimbali katika wilaya hiyo.

"Mtoto aliye chini ya miaka mitano kisheria inabidi awe katika kituo cha kulelea watoto, lakini anawekwa katika eneo linaloridhisha?" Aliongeza.

Kadhalika, alibainisha kuwa sheria hiyo ilianzishwa kutokana na sababu mbalimbali na changamoto za majukumu ya malezi na kwamba hivi sasa wazazi wengi kutowapatia malezi watoto hao muda wote.

Alisema vituo hivyo hupaswa kutoa huduma kama ambavyo mtoto yoyote huzipata pamoja na kumwongezea uchangamshi wa awali ili aweze kujitegemea.

Thomas alisema lengo la sheria hii ya uanzishwaji vituo hivi ni kumpa mzazi, mlezi kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa amani, na kwamba kundi la watoto wanaolelewa ni walio katika umri wa chini ya miaka mitano,

"Vituo vitaanzishwa katika makazi ya watu, lakini wengi wanachanganya hawajui tofauti ya nursery school na 'day care', vituo vinatakiwa ulinzi na usalama kwa watoto na ipatikane lishe bora," alisema.

Novemba 18, mwaka huu, saa 3:00 asubuhi kabla ya masomo kuanza, ukuta wa shule ya watoto wadogo Joy Unit Day Care, iliyoko mtaa wa Kisiwani, Kata ya Bonyokwa, Segerea, jijini Dar es Salaam, ulianguka na kusababisha vifo vya watoto watatu na sita kujeruhiwa.

Mmliki wa shule hiyo, Atuganile Mbosolelo, alishikiliwa kwa siku kadhaa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Ilala, akituhumiwa kumiliki shule bila kibali.

# Dk. Mpango ataka mashirika kujieleza kwa mapato kiduchu

**Na Benny Mwaipaja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ametoa siku tisa kwa wakuu wa taasisi na mashirika ya umma kujieleza kwa nini hawajachangia mapato kiduchu kwenye mfuko mkuu wa serikali. Pia amewataka kujieleza kuwa nini wameshindwa kuchangia huduma za kijamii pamoja na kutozingatia ukomo wa matumizi ya asilimia 60 ya mapato ghafi ya taasisi na mashirika yao kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Wizara hiyo, agizo hilo linaanza kutekelezwa kuanzia Desemba 22 hadi 31, mwaka huu. Dk. Mpango alitoa maagizo hayo jijini Dodoma juzi, alipokutana na wakuu wa taasisi za serikali na mashirika ya umma 236, ikiwa ni mwendelezo wa mikutano yake ya kikazi na taasisi mbalimbali za serikali, ili kutoa mwelekeo mpya wa utendaji wa taasisi hizo hususan kuimarisha na kuongeza mapato ya serikali.

Hivyo, Dk. Mapango alimwagiza Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka, kuhakikisha taarifa hiyo ya maandishi kutoka kwa wakuu hao wa taasisi inamfikia Desemba 31, na kutangaza kufuta likizo za sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwa viongozi hao ili watekeleze maelekezo yake.

Alifafanua kuwa Kifungu cha 47 cha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2015 na kifungu cha 8 cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 iliyorekebishwa mwaka 2015, kinazitaka Taasisi na Mashirika ya Umma kuchangia asilimia 15 ya mapato ghafi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini bado kuna taasisi ambazo zinachangia chini ya kiwango kilichowekwa kisheria, zingine kutokutoa kabisa.

Dk. Mpango alisema kuwa Kifungu cha 46 (1) cha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2015 na Kifungu cha 10A cha Sheria ya Msajili wa Hazina iliyorekebishwa mwaka 2015, kinaweka ukomo wa gharama za uendeshaji kwa taasisi na mashirika ya umma yasiyo ya kibiashara kutozidi asilimia 60 ya mapato ya ghafi, lakini bado kuna taasisi na mashirika ya umma zinavunja sheria hiyo.

Aidha, Dk. Mpango aliwaagiza wakuu hao wa taasisi kuhakikisha kuwa wanapunguza matumizi yasiyo na tija na yasiyo ya lazima, ikiwamo misafara mikubwa ya watendaji na wajumbe wa bodi kutembelea miradi.

Alisema idara zote zinazokusanya maduhuli, na halmashauri zote lazima zifanye jitihada zaidi kuongeza ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ili kuwezesha kutekeleza miradi hiyo kwa kutumia fedha za ndani kwa kiwango kikubwa, kwamba mambo hayo yatafanikiwa endapo watendaji hao wataacha kufanyakazi kwa mazoea.

Pia Mpango alimpongeza Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka kwa kusimamia na kuwezesha urejeshwaji wa mali za serikali, kupitia Kamati Maalum ya Uhakiki wa Mali za Serikali, ambazo zilikuwa zinamilikiwa na watu binafsi bila kufuata sheria na taratibu.

Alisema mali hizo za serikali zilikuwa zinamilikiwa na baadhi ya watu wasio waaminifu bila kuwa na hofu na kwamba zoezi la kutambua na kurejesha mali za serikali zilizoko kwenye mikono isiyohusika ni endelevu.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na.19 cha sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni Na. 17 (4) ya Kanuni za Petroleum (Wholesale, Storage, Retail and Consumer Installation Operations), Gazeti la Serikali Toleo Na. 380 la 2018)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea ombi la kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | Efficient Freighters (T) Ltd – Tunduma |
| **Nambari ya Leseni:** | PRL-2020-271 |
| **Mahali Kituo kilipo:** | Plot. No. 15 Block F- Mpamba Tunduma Mjini |
| **Jina linalopendekezwa:** | Effica Oils Ltd |
| **Mmiliki wa awali:** | Efficient Freighters (T) Ltd- Tunduma |
| **Mmiliki mpya:** | Effica Oils Ltd |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-3, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz



PASS
PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

## PUBLIC NOTES

Date: 21/12/2020

To: All Tanzanian Local Fundis/Building Contractors

On 21st October 2020, PASS Trust posted an advertisement of Request for Proposal with the heading **"PROPOSED CONSTRUCTION OF OFFICE BUILDING FOR PASS AIC SUA – MOROGORO"**, the advert was posted on PASS website and on newspaper with a submission deadline of 17th November 2020

We regret to inform our bidders that we have experienced some Technical challenges with the submitted proposals, so we request all bidder who had submitted their proposals through our website to resubmit them by email to procurement@pass.or.tz by 31st December 2020.

**Managing Director,**
PASS Trust, Dar es Salaam,

## Jaji Mwangesi Kamishna Maadili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. John Magufuli amemteua Sivangilwa Mwangesi (Jaji wa Mahakama ya Rufani) kuwa Kamishna wa Maadili.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa jana, ilisema Mwangesi ameteuliwa kushika wadhifa huo baada ya Jaji wa Mahakama ya Rufani mstaafu Harold Nsekela, kufariki dunia.

Taarifa hiyo ilisema uteuzi wa Jaji Mwangesi umeanza jana na ataapishwa leo saa 4:00 asubuhi, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

## Maganga ateuliwa Mkurugenzi REA

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Wakala wa Nishati Vijijini (ERB) imemteua Mhandisi Amos Maganga kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala huo kuanzia Desemba 16, mwaka huu.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa jengo la PSSSF, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Wakili Julius Kalolo, alisema uteuzi huo umefanyika kwa mujibu wa sheria.

"Kwa mamlaka Bodi iliyopewa kwa mujibu wa kifungu cha 25(1) cha Sheria Namba 8 ya Nishati Vijijini ya mwaka 2005, imemteua Mhandisi Amos Maganga kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Wakala," alisema.

Wakili Kalolo alisema majukumu makubwa ambayo wanamkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa REA ni pamoja na kuhakikisha vijiji vyote ambavyo havina umeme vinapelekewa nishati hiyo kabla ya Desemba, 2022 na kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo havina umeme.

Kabla ya uteuzi huo, Mhandisi Maganga alikuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA.

Mhandisi Maganga ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika sekta ya nishati na ameshika nyadhifa mbalimbali tangu alipokuwa ameajiriwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Alisema bodi inaomba ushirikiano kutoka kwa wadau wote ili kumwezesha Mhandisi Maganga kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya wakala.



Jengo la vyoo vya Shule ya Sekondari mpya ya Kigera, iliyopo Kata ya Nyakatende, Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, likiwa katika hatua ya kupauliwa. Shule hiyo inatarajiwa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wanne mbaroni tuhuma kumpiga dereva wa lori

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATU wanne ambao ni abiria waliokuwa wakisafiri na basi la Frester lenye namba za usajili T.915 CGU kutoka wilayani Kahama mkoani Shinyanga kwenda jijini Mwanza, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga kwa tuhuma za kumshambulia dereva wa lori, Emmanuel Nobert wakidai kutaka kuwasababishia ajali.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu salamu za sikukuu za mwisho wa mwaka na mwaka mpya kwa wananchi wa mkoa huo. Alisema katika tukio lililitokea Desemba 21 mwaka huu, katika Kijiji cha Samuye wilayani Shinyanga na kuzagaa mitandaoni likionyesha abiria wa basi wakimshambulia dereva wa lori kwa tuhuma za kutaka kuwasababishia ajali. Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Joyce Charles, Athumani Mussa, Christophe Rangati na Mwita Chaguche ambaye ni dereva wa basi la Frester, wote wakishikiliwa kwa tuhuma za kumshambulia na kumpiga dereva wa lori, Emmanuel Nobert. "Chanzo cha mkasa huo ni dereva wa basi la Frester kumfanyia vurugu dereva wa lori hilo kwa kuanza kumbana ubavuni ili ampishe awahi kupimwa uzito kwenye mizani ya Tinde, lakini dereva huyo wa lori aligoma na kisha kupimwa gari lake uzito na kuanza kuondoka kwenda jijini Mwanza akitokea Moshi," alisema Magiligimba.

"Lakini lori hilo lilipokuwa njiani kuelekea Mwanza, dereva wa basi la Frester baada ya kumaliza kupimwa uzito, alilikuta lori hilo njiani na kisha kulibana upande wa kushoto, na kumwonyeshea dharau kuwa licha ya kumnyima kuwahi kupimiwa uzito kwenye mizani, sasa amemkuta njiani ndipo dereva wa lori aliposimama," alisimulia.

Alisema kuwa baada ya dereva huyo wa lori kusimama, ndipo dereva wa basi, akisaidiwa na abiria hao, wakaanza kumshambulia dereva huyo wa lori kwa kumpiga ngumi na mateke.

Alisema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi wa tukio hilo kukamilika.

# Udanganyifu mitihani wamwibua Ndalichako

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema mwalimu yeyote atakayebainika kujihusisha na udanganyifu wa mitihani adhabu yake ni kufukuzwa.

Prof. Ndalichako, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati akifunga mkutano mkuu wa mwaka wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA).

Alisema suala la udanganyifu kwenye mitihani hivi sasa linaonekana kurudi kwa kasi, hivyo mwalimu yeyote atakayebainika kushiriki, hakuna adhabu nyingine zaidi ya kufukuzwa kazi.

"Suala la udanganyifu wa mitihani katika shule haliwezi kufanikiwa kama mkuu wa shule hajahusika. Sasa niwaonye wakuu wote kuwa atakayehusika nitahakikisha nakula naye sahani moja na adhabu yake ni kufukuzwa kazi na si vinginevyo," alisema.

Pia alisema ni aibu kwa mkuu wa shule kushirikiana na wanafunzi kufanya vitendo vya udanganyifu wa mitihani.

"Unakuta baadhi ya shule darasa zima limefanya udanganyifu. Hii haiwezi kutokea bila mkuu wa shule kushiriki, hivyo niwaonye wakuu wangu kuacha tabia hii ili kama mwanafunzi mwenyewe kaamua kufanya udanganyifu afanye hivyo.

Wako wengine wanajichora majibu hadi kwenye mapaja atajua mwenyewe atakavyojitetea maana yake mwizi ni yule atakayekutwa na kidhibiti," alisema.

Alisema udanganyifu wa mitihani umekuwa ukilitia aibu taifa na wakuu wa shule wanaohusika katika kufanikisha uovu huo.

"Unakuta mkuu wa shule anafanya maswali ya wanafunzi na kutuma kwa njia ya simu na wengine wanaingia hadi kwenye vyumba vya madarasa ya mitihani kwa njia za wizi na wasimamizi wakija wanaruka kwenye madirisha.

Sasa huyo ni mkuu wa shule au mhalifu? Alihoji Ndalichako.

Alisema ni jambo la kusikitisha kwa wakuu wa shule ambao wanashiriki katika udanganyifu kwa kuwa ni kuihujumu serikali ambayo imewekeza kiasi kikubwa cha fedha kugharamia mpango wa elimu bila malipo.

Ili kuondokana na tabia hiyo, alisema walimu wanatakiwa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wakati wote wanapokuwa shuleni kwa kuwa hiyo ndiyo njia sahihi ya kuongeza ufaulu.

Kadhalika Ndalichako, alisema suala la udanganyifu wa mitihani kama halitachukuliwa hatua za haraka, litakuwa na madhara makubwa kwa taifa.

"Hivi sasa hadi vyuo vya (mafunzo ya ufundi stadi) VETA wameanza kujihusisha na udanganifu wa mitihani. Niwapongeze sana (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) TAKUKURU ambao waliwakamata walimu na wanafunzi kwa kushiriki kufanya udanganyifu," alisema.

Kutokana na hali hiyo, amemwagiza Mwenyekiti wa Bodi ya VETA, kuwafukuza kazi wote walioshiriki kwenye udanganyifu wa mitihani kwa kuwa hawafai tena kuwa watumishi.

Pia aliomba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuacha kufanya uamuzi wa haraka ya kuwavua madaraka wakuu wa shule zinazofanya vibaya kitaaluma bali wafanye uchuguzi kwanza ili kubaini tatizo.

TANGAZO

QNET

# QNET ANAZUNGUMZA NA BIASHARA YAKE NCHINI TANZANIA

Hivi karibuni QNET imekuwa chini ya uchunguzi wa vyombo vya habari juu ya biashara na shughuli zake nchini Tanzania. Tunachukua fursa hii kufafanua msimamo wetu. Tunaahidi na kurudia kujitolea kwetu kwa wateja wetu nchini Tanzania kuhusiana na kuendesha biashara zetu kulingana na sheria za eneo.

**Kuhusu QNET**

QNET ni ya kimataifa ya biashara ya msingi inayouza moja kwa moja kampuni iliyoko Hong Kong. Kupitia bandari yetu ya e-commerce www.qnet.net, tunauza bidhaa bora za hali ya juu za afya, ustawi, na mtindo wa maisha kwa wateja kote ulimwenguni tangu 1998. Mbali na kutoa bidhaa nzuri, QNET pia inatoa fursa ya kuuza moja kwa moja kwa wateja kwa wateja ambao wanataka kuwa wasambazaji wa bidhaa zetu na kupata tume wakati marejeleo yao yanunua bidhaa kutoka QNET.

**QNET inawataja wasambazaji hawa kama Wawakilishi wa Huru (IRs).**

**Uuzaji wa moja kwa moja ni nini?**

Uuzaji wa moja kwa moja ni njia ya uuzaji na kuuza bidhaa na huduma moja kwa moja kwa watumiaji, katika nyumba zao au mahali pengine popote mbali na majengo ya rejareja ya kudumu. Uuzaji kama huo unasababishwa sana na uelekezaji wa neno-kwa-kinywa. Bidhaa zinazouzwa na kampuni za kuuza moja kwa moja zina huduma za kipekee, ni za kipekee sana na hazipatikani katika maduka makubwa au maduka ya idara.

Sekta ya kuuza moja kwa moja imekuwa mfano mzuri wa uuzaji-msingi wa uhusiano na mauzo kwa zaidi ya miaka 150. Takriban watu milioni 100 ulimwenguni wanahusika katika tasnia hii kwa uwezo wa muda wote na wa wakati wote.

**Mfano wa Biashara wa QNET**

Biashara ya QNET inachanganya viwanda viwili vikubwa pamoja, ambayo ni: e-commerce na uuzaji wa moja kwa moja. Mtu yeyote, wa umri halali, anaweza kununua bidhaa kutoka QNET na kuchagua kuchukua fursa ya kuwa IR. Wakati IR inapowasilisha bidhaa zetu kwa wengine kwenye bandari yetu ya e-commerce na kufanya uuzaji mzuri, wanapata kamisheni kutoka QNET.

Kwa sababu ya fursa ya biashara isiyo na mipaka na msaada mkubwa uliotolewa na QNET kwa IR kwa suala la mafunzo, zana za biashara, msaada wa wateja, na ofisi kamili ya mkondoni kuwasaidia kufuatilia mauzo na mapato yao, wafanyabiashara wengi wanaotamani wanaona hii kuwa fursa ya kuvutia kupata kipato cha nyongeza bila hitaji la kuwekeza katika vichwa vya kazi.

**Biashara ya QNET nchini Tanzania**

Kama biashara ya kimataifa ya e-commerce, QNET imekuwa ikisafirisha bidhaa kwa wateja wa Tanzania kwa miaka kadhaa sasa. Walakini, ni tangu tu mwishoni mwa 2017 ambapo wateja wetu wengi wamekuwa IR ya bidhaa zetu.

Mara tu QNET ilipoanza kupokea usajili thabiti kwenye bandari yetu ya e-commerce kutoka kwa Wawakilishi wa Independent (IRs) nchini Tanzania, tulishirikiana na shirika la karibu huko Dar es Salam kutuwakilisha kama wakala wetu wa ndani na kwa busara kushughulikia uingizaji na forodha zote idhini ya bidhaa, malipo ya ushuru unaofaa, na usimamizi wa hesabu za hisa Mpangilio huu uliendelea hadi Covid19 ilipofikia viwango vikali vya marehemu.

QNET kwa sasa inatafuta kuanzisha LLC ya kibinafsi nchini Tanzania, hata hivyo mchakato huu umecheleweshwa kwa sababu ya vizuizi vya kusafiri vinavyoendelea kama matokeo ya Covid-19.

Kujitolea kwa QNET kwa Tanzania

QNET inatambua kabisa umuhimu wa Tanzania katika eneo la Afrika Mashariki na ina nia ya kuimarisha uwepo wetu nchini wakati ikionyesha kujitolea kwetu katika ukuaji na maendeleo ya uchumi wa ndani.

Sambamba na hili, hivi karibuni tumezindua laini mpya ya vito chini ya kitengo cha bidhaa za kifahari kwa kutumia vito vya vito vya Tanzanite kutoka Tanzania ambavyo vinauzwa ulimwenguni kupitia jukwaa letu la e-commerce.

Kwa karibu miaka miwili sasa, mkono wa CSR wa QNET, RYTHM Foundation imekuwa ikiunga mkono shirika lisilo la faida la kujenga visima vya maji katika mkoa wa Iringa ambavyo vinatoa ufikiaji wa maji safi ya kunywa kwa maelfu ya wanakijiji. Msingi pia umefadhili kuanzisha shamba la ekari 50 ambapo karanga za macadamia na parachichi hupandwa, na wanakijiji wamefundishwa mbinu za kilimo za kisasa ambazo huwapatia riziki. Mapato kutoka kwa uuzaji wa mazao hurudi kwa jamii kusaidia kutunza visima vya maji katika mkoa huo.

Kwa kuongezea hii, QNET imekuwa ikijishughulisha mara kwa mara na jamii ya karibu kupitia mipango kadhaa ya ardhini. Tumeandaa maonyesho ya bidhaa kuonyesha bidhaa na huduma zetu, tumefanya majadiliano ya meza ya media ili kuwasilisha kampuni na modeli yetu ya biashara, tumechangia kikamilifu kwa idadi kadhaa ya misaada wakati wa mwezi wa Ramadhani kwa miaka kadhaa iliyopita.

Tunachukua fursa hii kuwahakikishia wateja wetu na mamlaka kwamba QNET imejitolea kuendelea na kufanya biashara zetu kwa kufuata sheria na kanuni za Tanzania. Daima tunabaki kupatikana kushughulikia maswali yoyote yanayotokea na tunaweza kuwasiliana kupitia habari ya mawasiliano kwenye wavuti yetu.

***ASANTE, TANZANIA! TUPO HAPA KUKUTUMIKIA.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Likizo isitumike kukeketa, unyago

**NI** mwisho wa mwaka ambao mabinti wa darasa la saba na wale wa sekondari wamehitimu masomo yao, wengine wakitarajiwa kujiunga na elimu zaidi.

Uwepo wa watoto au wanafunzi hao wakati huu wa likizo unawashawishi wazazi na walezi kuwacheza ngoma na wengine hata kuwakeketa.

Lakini, zama hizi ambazo kila mmoja amejua umuhimu wa elimu na serikali ikigharamia elimu msingi ni vyema mabinti wakaachwa wakasoma, ili kupata elimu na maisha bora.

Hivyo, tunaona kuwa kuna kila sababu ya wazazi na walezi kuachana na utamaduni na mila zinazowaponza wasichana hasa hizo za kuwacheza ngoma za unyago na hata kuwakeketa.

Tunatoa tahadhari wakati huu wa likizo kwa sababu wasichana hao wanaweza kuwa wanakaribia au wameshapevuka au kufikia umri wa kuvunja ungo.

Tunaona kuwa kubadilika na kuachana na mila hizo ni jambo la msingi kwa sababu mabinti hao ni wadogo na wengi wako shuleni na wanasoma na kila mmoja anatazamia kufanikiwa kupitia elimu si kukeketwa, kuozwa au kupata mimba utotoni au kuanza kushiriki matendo yasiyo na maadili akiwa na umri mdogo.

Tunaona kuwa kuwacheza ngoma wakiwa bado masomoni kunawaathiri kisaikolojia na na mihemko ya kimwili na huenda kwa kiasi kikubwa kukasababisha washindwe kuendelea na shule.

Ni vyema tutunze afya za watoto wetu na kuachana na masuala yanayowaharibia maisha yao.

Tunawahimiza na kuwataka wazazi na walezi kuachana na mila hizo potofu za kuwacheza ngoma watoto wa kike wakiwa bado wanasoma kwa masuala yasiyo na tija.

Kimsingi kwa makabila mengi na hasa ya pwani msichana akichezwa ngoma anaandaliwa kuolewa. Vivyo hivyo akikeketwa hilo ndilo lengo kuwa awe mwali anayesubiri kufunga ndoa, hivyo wadau wa elimu na viongozi wa serikali washiriki kikamilifu kupinga mila hizo potofu.

Ili kuwalinda watoto wa kike ili wasome tunaona kuwa kuna umuhimu wa kufanya jitihada za kupeleka mapendekezo ya kutunga sheria ndogo zitakazopiga marufuku mabinti wanaosoma kuchezwa ngoma.


Wazazi na walezi na jamii isubiri hadi wanapomaliza masomo tena kwa kuwauliza iwapo wako tayari kufundwa na hata ikibidi walimu, wazazi, serikali, walezi na wadau kushirikiana kupinga masuala ya mila zisizo na tija na kuhimiza kutoa elimu bora kwa watoto. Tunashauri wakati wa likizo uwe muda wa kutafakari njia bora za kuongeza ufaulu kwa watoto wakike ili unapande zaidi na wawe na nidhamu na kuepuka masuala ya udanganyifu hasa wakiwa shuleni.

Wakati serikali ikitekeleza majukumu ya kuhakikisha kunakuwapo na walimu kulingana na mahitaji ya shule na kushughulikia maslahi ya walimu kwa wakati, kuwapa motisha mbalimbali kwa mujibu wa miongozo ya utumishi wa umma, wazazi, walezi, wadau na mabinti watafute masuala yenye tija badala ya ngoma za unyago na kutafuta kukeketwa.

Tunaamini kuwa wadau mbalimbali wataunga mkono juhudi za kuondokana na mila potofu zinazokwamisha elimu ya wasichana na kuwahamasisha wazazi na walezi ili wawe chachu ya mafanikio katika kuinua kiwango cha ufaulu cha wasichana kwa kushirikiana na walimu ili kuijenga nidhamu ya watoto wao.

Kwa hiyo tunawasihi wazazi kuachana na utamaduni na mila ambazo zinawakwaza watoto kusoma na wawe mstari wa mbele kuwalinda na kuwatunza mabinti wakati wote wa likizo wakiwafundisha kujitambua ili waweze kujua mema na mabaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tushikamane kuwaibua yatima na wajane shimoni, wana mchango

Na Irene Philemon

**KWANZA** nianze neno la kutakiana heri kwa siku hii maalum ya kiimani, kihistoria na kijamii kwa ujumla.

Hapa naamua kuwasilisha mtazamo usio mbali na maudhui ya jumla ya siku hii, lakini ndani ya maisha ya jamii yetu. Nianze kwa kuhoji msamiati wenyewe mkuu, je, yatima ni nani?

Huyu ni mtu aliyekosa wazazi wote wawili na anaweza kuangukia umri wowote. Katika uhalisia wa binadamu, hakuna anayependa ama kubeba hadhi hiyo au au hata kuitwa hivyo katika maisha yake ya kila siku. Huwa analazimika kuangukia hapo.

Mjane je? Huyo ni mwanamke aliyefiwa na mume. Kwa ujumla, wote kwa pamoja na yatima, ni watu wenye mahitaji binafsi tofauti.

Je, wanayapata yote katika maisha yao ya kila siku? Kuna wengine kati yao wana matatizo wasioweza kuyakidhi, ikiwamo ya masomo.

Hawa ndio tunaowaangalia kiujumla kama wanapata elimu, kwa namna gani na nani atakayewafikisha huko? Tunahitaji kuwasaidia kwa sabau hakuna wa kuwaelekeza pasipo mimi na wewe.

Sasa hapo ndipo tunapowajibika kuwaangalia kama ni yatima wasio na msaada. Sisi ndio wa kuwapeleka mahali husika wanakoweza kupata mahitaji ya msingi na kupiga hatua badaaye katika maisha yake.

Tuwasaidie kwa jumla wanaohitaji msaada, pia wote wasioweza kupata mahitaji yao. Msaada kwao una sura pana, kwani hata tukiwasogeza wanyonge hao panapopatikana cha kuwasaidia, tayari kunazaa maana kwao.

Wanajamii tunaoishi nao kwa karibu ndio wa kwanza katika utoaji msaada ndani ya sura kuu, kwamba sisi ndio tunaoishi nao. Pia, ndio tunaojua kwa namna moja au nyingine wanavyoamka, kuvusha siku hata kufikia kulala.

Sasa ni jukumu letu pamoja kuwasadia waishi katika mazingira mazuri na waweze kupata hayo ya msingi. Najaribu tena kuhoji katika maoni yangu, nafasi ya kiserikali inawasaidiaje hawa wajane na yatima?

Kuwasaidia yatima kupata elimu, ndio kuwasaidia katika hatua zaidi ya kimaendeleo ndani ya maisha yao ya baadaye, kwani taifa linawahitaji wasomi na nguvu kazi katika maendeleo ya taifa la baadaye. Hiyo ni katika kujibu swali la majukumu kitaifa baadaye, hata panapozungumziwa nafasi kuu mfano hai ni fursa za urais.

Wote hao wawili wanahitaji mchango mkubwa wa kushikwa mkono kutoka serikalini, kwani kuna maeneo muhimu iwe kisera, kisheria, kibajeti au uamuzi wa namna fulani.

Ni wazi inawezekana isiwe msaada wa fedha, hata kuwapo faraja ya kiserikali yenye nafasi kubwa ya kuleta mageuzi makubwa kwao, pale wanagundua ya kujiona hawajasahaulika kitaifa.

Kwa kufanya hivyo, kuna hilo linalojisikia wanyonge wanapogundua hawajasahaulika kutoka mamlaka za umma na kitaifa, hapana shaka inazaa fukara kubwa kwao.

Kwa kufanya hivyo, ni jambo linalounda dhana chanya kwamba watu hawa watajivunia serikali yao licha ya majukumu mengi iliyo nayo, bado haijapoteza nafasi ya kuwaona kada kama yatima na wajane, kuwa nao pamoja.

Serikali inapochukua nafasi kuhudumia makundo hayo, inabeba maana kwamba ni fursa ya kufungua milango hata walio katika kada hizo hawakupata fursa ya kusoma wakaelimike.

Kuwasaidia yatima kupata elimu, ndio kuwasaidia katika hatua zaidi ya kimaendeleo ndani ya maisha yao ya baadaye, kwani taifa linawahitaji wasomi na nguvu kazi katika maendeleo ya taifa la baadaye.

Hiyo ni katika kujibu swali la majukumu kitaifa baadaye, hata panapozungumziwa nafasi kuu mfano hai ni fursa za urais.

Niseme katika upande wa pili wa shilingi, wajane hao wanapewa darasa la mafunzo kujua nao wana nafasi ya kujenga taifa na hata kuwa na tija kwa manufaa ya umma.

Ushauri wangu serikalini, daima isiwasahau wanyonge hao tajwa katika umuhimu mojawapo nililosisitiza wa elimu. Tusisite kuwasaidia watu hawa, kwani kwa pamoja tunaweza kuwasaidia yatima na wajane.

HABARI KITAIFA

# Waziri atangaza msako walimu wa kigeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amesema kuwa serikali itafanya uhakiki katika shule zote za msingi, sekondari vyuo vya kati na vyuo vikuu, kubaini walimu wanaofanya kazi bila kuwa na vibali.

Uhakiki huo, amesema utafanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Ajira na Vijana ambao ndio wanaohusika katika utoaji wa vibali vya kazi kwa raia wa kigeni.

Prof. Ndalichako, alibainisha hayo juzi alipokuwa akifunga mkutano mkuu wa mwaka wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSSA).

Alisema uhakiki huo unakuja kutokana na sekta ya elimu kuendelea kuwa kichaka cha kuficha raia wa kigeni wanaofanya kazi nchini bila kuwa na vibali vya kazi.

"Nimeshaongea na Waziri (Jenista) Mhagama (anayeshughulikia Kazi na Ajira), tutafanya uhakiki wa kila shule na vyuo vyote, ili kubaini hawa ambao wanajificha na kuendelea kufanya kazi kinyume cha sheria. Naomba mnapotoka hapa mwende mkafyeke hivyo vichaka wanavyojificha maana tunakuja na hatutakuwa na huruma nao," alisema.

Prof. Ndalichako aliwataka wakuu wa shule hao kusimamia sheria za nchi na pindi wanapoona wamiliki wa shule wanaleta walimu kutoka nje ya nchi bila kufuata utaratibu.

"Wakuu wa shule tunaomba mtoe taarifa za waajiri wenu ambao wamekuwa wakikiuka sheria za nchi na kuleta walimu nchini kuja kufundisha bila ya kufuata sheria za nchi," alisema.

Ndalichako alisema katika uongozi wake hataruhusu vitendo hivyo kuendelea bali atahakikisha vinakomeshwa kwa mujibu wa sheria za nchi na wahusika kuchukuliwa hatua kali.

Sambamba na hilo, alizitaka shule binafsi kuahakikisha kuwa zinafuata kanuni za usajili na kuacha tabia ya kujichukulia hatua bila kushirikisha serikali.

"Kumeibuka tabia ya shule imesajiliwa kama ya kutwa mara ya muda kidogo inakuwa ya bweni bila hata kufuata taratibu eti tuu kwa sababu imejenga kajengo kamoja na kukaita bweni," alisema Ndalichako.

Ndalichako alizionya shule binafsi ambazo zimekuwa na tabia ya kuwabagua baadhi ya wanafunzi kwa madai kuwa hawana uwezo na kuzitaka kuacha mara moja tabia hiyo.

# TANESCO yaagizwa kuunganishia wateja wote waliolipa

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

NAIBU Waziri Wizara ya Nishati, Stephen Byabato, ameliagiza Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), mkoani Kagera kuwaunganishia umeme wateja wote waliolipia gharama za kuunganisha kufikia Januari 31, mwakani.

Alitoa agizo hilo jana baada ya kusikiliza matatizo na malalamiko kutoka kwa wateja wa shirika hilo katika maeneo ya Muleba, Missenyi, Karagwe na Bukoba mjini.

Alisema nguzo za umeme zipo, mita na nyaya zipo za kutosha zinazidi mahitaji, huku akitoa onyo kwa watakochelewesha huduma hiyo kwa wateja wao kuchukuliwa hatua.

Aliwataka watendaji wa TANESCO wananchi 887 wa Mkoa wa Kagera waliokamilisha taratibu zote za kuunganishiwa umeme kupata huduma hiyo ndani ya muda aliotoa.

Alitoa pongezi kwa watendaji wa shirika hilo kwa kazi waliyoifanya mkoani Kagera kwa kufikisha umeme wa REA, katika vijiji 156.

Alisema REA awamu ya tatu inayotarajiwa kuanza mwezi Februari 2021, itaenda katika vijiji 115.

Alisema lengo la serikali ni kupeleka huduma bora kwa wananchi na kufikiwa na huduma hiyo kwa wakati.

Alisema kwa sasa Tanzania inazalisha umeme megawati 1,602, huku matumizi yakiwa 1,177 na ziada.

Alisema miradi ya umeme inayoendelea kutekelezwa ukiwamo wa Mwalimu Nyerere ambao ukikamilika utazalisha megawati 2,115 na mradi wa Rusumo ambao utazalisha megawati 80 na Tanzania kupata megawati 27.

Msimamizi wa miradi ya REA, Kanda ya Ziwa, Ernest Makale, alisema mradi huo ulianza mwaka 2008, lengo lilikuwa kupeleka umeme makao makuu ya wilaya na maeneo ambayo yalipitiwa na miundombinu.

Makale alisema awamu ya pili ilikuwa kupeleka umeme kila kata, lakini kata nyingine hazikupata nishati hiyo kutokana na tatizo la bajeti kwenye awamu ya tatu ambayo kila kijiji kilitakiwa kuwa nao.

Alisema kutokana na hali hiyo waliamua kuanza mzunguko wa kwanza ambao unakamilika Desemba 31, mwaka huu.




The Guardian Nipashe
MWANGA WA JAMII

TWO UNBEATABLE DEALS IN ONE PLACE

Free Delivery at your Door Step + more than 20% off on 1 year upfront Subcription

| Number of Dailies | Cover Price (Tsh) | Offer Price(Tsh) | Your Saving (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 1 Months | 26,000/= | 24,000/= | 2,000/= |
| 3 Months | 79,000/= | 70,000/= | 9,000/= |
| 6 Moths | 157,000/= | 130,000/= | 27,000/= |
| 1 Year | 314,000/= | 250,000/= | 64,000/= |

Please mention the start date from when you want to receive your subscription

**For enquiry**,Please contact Subcription Supervisor - **Sophia Lema**

+255713852323

**Email:** subscription@guardian.co.tz

Offer valid from 1st Dec 2020 to 31st Dec 2020

Terms & Condition Apply



## Serikali kutoa kipaumbele ajira walimu

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

SERIKALI imesema inatambua tatizo la upungufu wa walimu shuleni ni la kitaifa na hatua mbalimbali zinachukuliwa kwa awamu kutatua kila fursa ya ajira inapotolewa.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alisema hayo wakati akipokea taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, katika ziara ya siku tatu mkoani humo na kwamba asilimia 65 wanaonyesha zaidi matunda mazuri ya ufaulu kwa watoto.

"Kwa sababu tunafahamu changamoto ya mwalimu ni ya kitaifa na hatua zinaendelea kuchukuliwa kwa awamu, sisi tutaendelea kufuatilia na kulifanyia kazi hilo kwa kila fursa inapotokea za ajira basi nasi kama mkoa au nchi kwa ujumla tutaendelea kuboresha," alisema Dugange.

Alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Njombe kupitia kamati yake kufanya tathmini sababu ya kushuka kwa ufaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Dk. Dugange alisema tathmini hiyo inapaswa kujumuisha mazingira ambayo yamekuwa kikwazo cha kutofanya vizuri na njia mbadala kipi kifanyike ili kuboresha sekta ya elimu na mwakani waanze vizuri na kupandisha ufaulu.

Alisema Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa iliyokuwa inafanya vizuri kwenye sekta ya elimu kwa miaka mingi, hivyo tathmini ikifanyika vizuri itawezesha kuinua kiwango cha elimu mkoani hapo.

## UNFPA yatoa msaada mashine ultra sound

**Na Happy Severine,**
BARIADI

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA), limetoa msaada wa mashine ya kupima magonjwa ya ndani ya mwili (Ultra sound) kwa hospitali ya mji wa Bariadi, mkoani Simiyu (Somanda), ikiwa ni mwaka mmoja tangu kifaa hicho kuibiwa katika hospitali hiyo.

Mashine hiyo yenye gharama ya zaidi ya Sh. milioni 30, imepokewa na mkuu wa wilaya hiyo na kukabidhiwa jana kwa uongozi wa hospitali hiyo kwa ajili ya wajawazito.

Agosti 5, 2019, mashine hiyo iliibwa katika hospitali ya wilaya kwenye wodi ya wajawazito na tangu ilipoibwa haijapatikana.

Akizungumza baada ya kupokea mashine hiyo, Mkuu wa Wilaya, Festo Kiswaga, alisema huduma za upimaji kwa wajawazito zimerejea hospitalini hapo baada ya mashine kupatikana na kuwataka watumishi wa hospitali hiyo kutunza vifaa tiba vinavyotolewa na serikali na wadau wa maendeleo.

"Tunawashukuru UNFPA kwa huruma yenu, mwaka mmoja uliopita iliibiwa Ultra sound hapa, lakini leo mmeleta nyingine tunawashukuru sana...lakini nina imani iliyoibiwa itarudi na hii ikipotea tutachukua hatua kali zaidi ya mwanzo," alisema Kiswaga.

Mratibu wa UNFPA Mkoa wa Simiyu, Dk. Amiri Batenga, alisema, tangu kupotea kwa mashine hiyo wanaopata shida ni wajawazito na wametoa mashine hiyo ili huduma za upimaji katika jengo hilo ziendelee.

Alisema hawaungi mkono upotevu na hawasitishi hatua zilizochukuliwa, lakini wanakabidhi tena mashine hiyo ili kusaidia wajawazito kubaini tatizo tumboni.

Mganga Mfawidhi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Dk. Judith Ringiya, aliishukuru UNFPA kwa msaada wa majengo pamoja na vifaa tiba vinavyotolewa katika halmashauri hiyo.

"UNFPA wamejenga wodi za wazazi tano za kisasa, jengo la upasuaji kituo cha afya Ngulyati na katika Hospitali ya Somanda tumekabidhiwa wodi ya wazazi pamoja na vifaa tiba vyote tunawashukuru sana...tunawaahidi mashine hii tutaitunza sana ili isaidie kinamama kuwafanyia uchunguzi," alisema Dk. Ringiya.

Alisema, baada ya mashine kupotea waliendelea kutumia nyingine ambayo ni ya kizamani iliyokuwapo hospitalini hapo na kwamba sasa watarahisisha upimaji wa wajawazito na huduma zitakuwa na ufanisi.



Balozi wa NMB, Nancy Sumari (kushoto), akimpigia simu mmoja wa washindi wa droo ya mwezi ya Mastabata iliyochezeshwa jijini Dar es Salaam jana. Washindi 12 walipatikana kwenye droo ya mwezi huu, ambao walijishindia simu ya Samsung Note 20 yenye thamani ya Sh. milioni 2.4. Kulia ni Ofisa Mkaguzi Kutoka Bodi ya Michezo ya kubahatisha, Pendo Mfuru na katikati ni Meneja wa Benki ya NMB Kitengo cha Kadi, Sophia Mwamwitu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yatahadharisha uvunjifu amani Krismasi, Mwaka Mpya

**Romana Mallya na Ndalike Sonda**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limewataka wananchi kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya kwa utulivu na kuwataka wajiepushe na vitendo vya uvunjifu wa amani.

Kamanda wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sikukuu hizo. Kamanda Mambosasa alisema jeshi hilo limejipanga kuhakikisha wakati wote wa sikukuu ulinzi unakuwa imara.

"Tumejipanga kuimarisha doria maeneo yote muhimu zikiwamo nyumba za ibada, fukwe za Bahari ya Hindi na tunawatadharisha watembea kwa miguu na madereva wa vyombo vya moto kuendelea kufuata sheria za usalama barabarani," alisema.

Pia aliwataka wazazi na walezi kuwa makini kwa kuwalinda watoto, ili kuepuka ajali zisizo za lazima kama kuzama majini.

Mkoani Simiyu, Jeshi la polisi limewataka wananchi watakaokwenda kwenye ibada ya mkesha wa Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya kuacha walinzi wa nyumba zao kuimarisha ulinzi kwenye makazi yao.

Kamanda wa Polisi mkoani Simiyu, Richard Abwao, akizungumza na Nipashe, alisema si vizuri kutoka wote nyumbani kwenda kanisani usiku na kuacha nyumba bila ulinzi.

Alisema jukumu la ulinzi siyo la Jeshi la Polisi pekee bali ni la kila mmoja na kwamba ni vyema kutoa ushirikiano kufanya ulinzi na kuwaonya wananchi wanaopanga kujihusisha na uhalifu kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wanaokwenda kwenye ibada ya mkesha wa Krismasi na Mwaka Mpya waache mtu nyumbani," alisema Kamanda Abwao.

Aliwataka wananchi kuwa tayari kutoa ushahidi wa watuhumiwa wa uhalifu watakapofikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake huku akiwaonya madereva wa vyombo vya moto kutotumia kilevi kama wataendesha vyombo vyao vya moto.

## Mbunge ashtukia udanganyifu miradi ya maji

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MBUNGE wa Jimbo la Sengerema, Hamis Mwagao (CCM), ameshtukia udanganyifu katika miradi ya maji jimboni kwake mkoani Mwanza na kuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kukagua mahesabu ya matumizi ya Sh. bilioni 26.05.

Mwagao alisema wananchi wamekuwa na maswali mengi ya matumizi ya fedha hizo baada ya miradi ya maji kukamilika na huduma kuendelea kuwa tatizo.

Akizungumza katika kikao cha kwanza cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mwanza kwa mwaka wa fedha 2020/2021, alisema miradi ya maji bado ina ubabaishaji kwenye jimbo lake.

Alitoa mfano wa mradi wa Buyagu ambao alisema ulianza mwaka 2014 na kugharimu Sh. bilioni 1.7, lakini hakuna matokeo mazuri ya upatikanaji wa huduma hiyo.


Mradi mwingine ni wa Katunguru ulioanza mwaka 2019 na kugharimu Sh. milioni 730 na Nyamazugo uliochukua Sh. bilioni 23 ambayo hadi sasa haujakamilika.

Kuhusu mradi wa Nyampande ulioanza mwezi Machi mwaka 2019 na kutakiwa kukamilika Oktoba mwaka huu, haujakamilika na umetumia Sh. bilioni 1.35.

"Miradi ya maji iliyopo Sengerema ni ya ujambazi tumezungumza na CAG na watu wake na leo hii nimezungumza kwenye kikao hiki tumekubaliana na SUWASA, MWAUWASA na RUWASA tunataka tuirudie kukagua kwani inatesa wananchi wakisikia Sh. bilioni 1.3 na Sh. bilioni 1.6 halafu hakuna maji wanaumia sana," alisema.

Vile vile, alisema kama wangekuwa wamechimba visima na wakaachana na miradi hiyo iliyokwisha, wananchi wangekuwa hawana shida ya maji. Alisema miradi ya mabomba ingepelekwa maeneo ya mjini, lakini vijijini watu wanataka wachote kwenye visima ambavyo havina gharama visivyozidi Sh. milioni 30.

"Nafikiri hili tutamshauri Rais Magufuli kwani tunaona watu wanaendesha magari kwa pesa zetu za maji hadi roho inauma, mradi wa maji Nyamazugo, Sengerema wa Sh. bilioni 23, unadaiwa una miaka mitatu umeshindwa kulipa deni la TANESCO la Sh. milioni 300," alisema.




Mkuu wa Masoko wa Benki ya Stanbic, Desideria Mwegelo (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa Mkuu wa Masoko wa Projekt Inspire, Ronnie Godfrey (katikati) pamoja na Meneja wa Projekt Inspire, Issa Ipiana (kushoto), kama msaada wa kuwezesha kambi ya vijana ya STEM inayoandaliwa na kampuni hiyo. Mchango huo ni moja ya harakati za benki kusaidia maendeleo ya vijana katika jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miaka 30 jela, viboko 6 kwa kumpa mimba mwanafunzi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Kenyenze, Innocent Mataba (32), kifungo cha miaka 30 jela na viboko sita kwa makosa mawili ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la tano mwenye umri wa miaka 16.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha makosa hayo pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Kiiza alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali kwa mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na vijana wengine wenye tabia za kubaka wanafunzi.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, James Pallangyo, ulipeleka mahakamani mashahidi watatu na vielelezo vitatu ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo.

Aidha, hakimu alisema mshtakiwa alimshawishi kwa kumrubuni mwanafunzi huyo kuwa atamuoa na kwenda kuishi Katoro kama mke na mume.

Alisema baada ya mwanafunzi huyo kugundua kuwa ni mjamzito alimweleza mshtakiwa, lakini aliukana ujauzito huo kwa madai kuwa siyo wake.

Alisema, mwanafunzi alirudi nyumbani kwao na kuendelea na masomo na wakati akiwa shuleni mwalimu alimbaini kuwa ana ujauzito na kumchukua hadi hospitali kwa vipimo na daktari alipomfanyia uchunguzi alibaini kuwa ana ujauzito wa miezi mitano. Hakimu Kiiza alisema mwanafunzi huyo alifukuzwa shule na taarifa zilipelekwa kwa wazazi wake ambao walimpeleka mtoto wao Kituo cha Polisi Geita na alipohojiwa aliyempa ujauzito huo alimtaja.Alisema mshtakiwa alikamatwa na katika mahojiano alikiri kufanya mapenzi na mwanafunzi huyo.

Hakimu Kiiza alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua upande wa mashtaka umethibitisha makosa hayo pasipokuacha shaka yoyote.

"Mshtakiwa mahakama hii inakutia hatiani kwa makosa uliyoshtakiwa nayo, pia mahakama hii inakutaka ujitetee ili iweze kukupunguzia adhabu," alisema hakimu.

Mshtakiwa huyo alinyamaza kwa muda na baadaye aliangua kilio. Hakimu Kiiza alisema mshtakiwa utakwenda jela miaka 30 na viboko sita ili iwe fundisho kwa jamii kwamba wanafunzi wapo kwa ajili ya kusoma na siyo kuingizwa kwenye masuala ya mapenzi.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, James Pallangyo, alidai kuwa tarehe na muda tofauti mwezi Februari, 2019 katika Kijiji cha Buseresere, Wilaya ya Chato, Mkoa wa Geita mshtakiwa alimbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi huyo.

# 'Walimu wanaofanya vizuri wateuliwe wakuu wa shule'

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ameagiza walimu wa shule zinazofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa wawe wanateuliwa kuwa wakuu wa shule na maofisa elimu kata.

Alitoa kauli jana, baada ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Msingi Mbirani na Shule ya Sekondari ya Kamagi, ikiwa ni ziara yake ya kuhamasisha ukamilishaji wa upungufu wa vyumba vya madarasa. Dk. Sengati alisema atamwagiza Katibu Tawala mkoa ili wanapotafuta walimu wakuu wa shule za msingi na wakuu wa shule za sekondari na maofisa elimu kata wachukue miongoni mwa walimu wanaotoka shule zinafanya vizuri.

Alisema lengo ni kutaka kuwa na viongozi wa shule na kata wanaofanyakazi kwa bidii na kwa uzalendo na walio tayari kujitoa, ili kuhakikisha shule wanazosimamia zinafanya vizuri.

Katika hatua nyingine Dk. Sengati aliwataka viongozi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, kufanyakazi usiku na mchana ili kuhakikisha wanamaliza upungufu wa madarasa na samani ili ifikapo Februari 28, mwakani wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wawe darasani.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Magiri, alisema wanakabiliwa na upungufu wa vyumba 10 kwa ajili ya wanafunzi wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza, mwakani. Alisema katika kukabiliana na tatizo hilo wameamua kuwa shule zote zenye upungufu wa vyumba vya madarasa zitatumia vyumba vya maabara na mabwalo kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kusomea.

Magiri alisema, lengo ni wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza waanze masomo ifikapo Januari mwakani.

Alisema katika mkakati wa muda mrefu, halmashauri imetenga Sh. milioni 30 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kujenga vyumba vitatu katika shule za Usunga, Tutuo na Igigwa.

Vile vile, alisema kupitia mpango wa lipa kulingana matokeo (EP4R), wametenga Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba sita vya madarasa na matundu 10 ya vyoo katika shule mbalimbali za sekondari.

# Faini wazidisha mizigo kuongezeka Januari

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

NAIBU Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, amesema kuanzia Januari mwakani, faini za wasafirishaji wa mizigo zitakuwa kubwa kudhibiti wanaozidisha uzito.

Alisema wasafirishaji wanatakiwa kuzingatia sheria na kanuni za barabarani kwa kupakia mizigo inayoendana na uzito wa gari hali inayochangia uharibifu wa barabara.

Kasekenya aliyasema hayo jana, baada ya ziara yake ya kikazi ya siku moja yenye lengo la kutembelea upanuzi mradi wa ujenzi wa barabara katika eneo la Vigwaza.

Alisema wasafirishaji wanatakiwa kupakia mizigo inayoendana na uzito wa magari yao na watakaokiuka watakumbana na faini zitakazoanza kutumika mwezi Januari mwakani.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Pwani (TANROAD), Yudas Msangi, alisema mradi huo ulioanza kutekelezwa Septemba, 2019 hadi kukamilika unatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 17.

# Madaba wapeleka kilio cha umeme TANESCO

**Na Neema Hussein,** MADABA

WAKATI Wizara ya Nishati ikijivunia kusambaza umeme kwa asilimia zaidi ya 80 katika maeneo mbalimbali nchini, hali ni tofauti kwa wakazi wa kijiji cha Lilondo, Jimbo la Madaba na wameliomba Shirika la Ugavi Umeme nchini (TANESCO) kufikisha nishati hiyo mtaa wanaoishi, ili waweze kutumia kwa ajili ya miradi ya maendeleo inayolenga kuwainua kiuchumi.

Wakitoa kilio chao mbele ya Mbunge wa Jimbo la Madaba, Joseph Mhagama, walisema katika utekelezaji wa mradi wa umeme vijijini (REA) awamu ya kwanza na pili, baadhi ya wananchi wameriukwa kwa kutounganishwa licha ya kulipa gharama zote na kufanya maandalizi muhimu yanayohitaji huduma hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake Lusitika Wella na Alex Mlelwa, walisema, umeme katika kijiji hicho umefika, lakini katika mtaa wa Msekenalo na ofisini hakuna nguzo hata moja, hali inayowakatisha tamaa ya kupata umeme siku za karibuni. Aliiomba wizara husika kuingilia kati suala hilo kwa kuwa linakwamisha juhudi za Rais Dk. John Magufuli ya kuunganisha umeme kwa kila mwananchi.

## CRDB yajumuisha Watanzania huduma rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imesema imelenga kuwajumuisha Watanzania 100,000 katika huduma rasmi za benki kupitia kampeni maalumu ya "Tupo Mtaani Kwako" ambayo ili kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utoaji huduma ikiwamo CRDB Wakala, SimBanking, Internet Banking na TemboCard.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha CRDB Wakala, Ericky Willy, alisema kampeni ya "Tupo Mtaani Kwako" imelenga kuwafikia zaidi ambao hawajafikiwa na huduma rasmi za benki, ili kuwawezesha kujumuishwa katika mfumo rasmi wa huduma za benki kutokana na takwimu kuonyesha asilimia 20 pekee ya Watanzania wanatumia huduma rasmi za benki.

Kampeni hiyo imefanyika katika mikoa 27 ya Tanzania Bara na Visiwani. Baadhi ya mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Masasi, Ruvuma, Songea, Njombe, Songwe, Iringa, Dodoma, Pwani, Tanga, Moshi, Arusha, Babati, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Musoma, Simiyu, Kagera na Unguja.

## Wananchi wapongeza ujenzi daraja Ulongoni

**Na Maulid Mmbaga**

WANANCHI wa Ulongoni B jijini Dar es Salaam, wameipongeza serikali kwa jitihada za kukamilisha ujenzi wa daraja ambalo ujenzi wake umekuwa wa kusuasua.

Daraja hilo linalounganisha Kinyerezi na Kata ya Gongo la Mboto, yenye wakazi 57,321 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, ujenzi wake umekuwa ukisuasua kutokana na maji ya mvua yaliyokuwa yakijaa eneo hilo na kusababisha shughuli za ujenzi kusimama na kuleta tafrani kwa watumiaji wa barabara hiyo hasa watumiaji wa vyombo vya moto.

Akizungumza na Nipashe, Omary Sudi, mmoja wa madereva bajaji, alisema tangu daraja hilo lisombwe na maji wanapata shida kupita eneo hilo kutokana na miundombinu kuwa mibovu.

Alisema baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa daraja hilo siku chache zilizopita, sasa linatia matumaini na kasi ya ujenzi inaridhisha.



Wakazi wa Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma wakisikiliza kampeni ya Tupo Mtaani Kwako inayoendeshwa na Benki ya CRDB ikiwa na lengo la kutoa elimu ya huduma ya kifedha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wamiliki vyombo usafiri watakiwa kulinda abiria

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WAMILIKI wa magari na pikipiki zinazotumika kusafirisha abiria wilayani Tunduru kwenda ndani na nje ya wilaya mkoani wa Ruvuma, wametakiwa kufanya matengenezo ya vyombo vyao ili kuwanusuru abiria na ajali.

Wajumbe wa Kamati ya Usalama Barabarani Wilaya ya Tunduru, walitoa ushauri huo katika kikao cha kujadili mipango mkakati wa kukabiliana na ajali za barabarani kilichofanyika juzi na kutahadharisha kuwa kama wataachiliwa waendelee kufanyabiashara zao kwa mazoea, abiria wataendelea kupoteza maisha na kupata vilema vya maisha.

Kamati hiyo pia imeridhia utekelezwaji wa mikakati mbalimbali iliyowekwa na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani ya kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto mara kwa mara, operesheni za barabarani, kusimamia sheria kwa kuchukua hatua bila kuwabambikizia makosa, kuandika faini kwa makosa hatarishi kuwakamata, kuwapiga pingu na kuwafikisha mahakamani madereva wote watakaobainika kuvunja sheria.

Wakichangia maoni kwa nyakati tofauti, baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo, Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Wendi Robert, mwakilishi wa madereva bodaboda, Aley Chilakwechi, walisema katika utekelezaji wa mpango mkakati, askari hao watoe elimu mara kwa mara kwa madereva na kufanya makongamano ya kudhibiti makosa hatarishi ikiwamo ulevi kwa madereva, kutoa adhabu kwa abiria aliyezidi kwenye gari na aliyekaidi maelekezo ya kufunga mkanda pamoja na adhabu kwa abiria wa pikipiki asiyevaa kofia ngumu.

Awali, akitoa taarifa ya matukio ya ajali katika kipindi cha miezi ya Septemba hadi Desemba, mwaka huu, Katibu wa Kamati hiyo, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Tunduru na Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Anosisye Mwaipopo, alisema jumla ya wananchi tisa wameripotiwa kufariki dunia katika matukio ya ajali zaidi ya 15 zilizotokea wilayani humo na kusababisha majeruhi kadhaa ambao wamepata ulemavu wa maisha.

Alisema katika uchunguzi uliofanywa na maofisa wa kitengo cha usalama barabarani, katika matukio ya ajali hizo walibaini kuwa chanzo chake ni ubovu wa vyombo vya moto pamoja na ukiukaji wa sheria za uendeshaji wa vyombo vya moto.

"Ajali ni kati ya maisha na kifo au ulemavu ambao umekuwa ukisababishwa na uendeshaji usiozingatia usalama wa abiria au ubovu wa vyombo vya moto," alisisitiza Mwaipopo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Athumani Nkinde, alisema usimamizi wa sheria kwa kutoa

## Wawekezaji viwanda wakaribishwa Sikonge

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amewakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya Tanzania kwenda wilayani Sikonge kujenga viwanda vya aina mbalimbali.

Alitoa kauli hiyo, jana na baada ya kukagua ujenzi wa kiwanda cha kati cha kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki wilayani Sikonge.

Dk. Sengati alisema, Wilayaya Sikonge imeonyesha utayari wa kupokea wawekezaji kwa kupima eneo la awali ukubwa wa hekta 8.8 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kati.

Alisema eneo lililopimwa lipo kando ya barabara na kumfanya mwekezaji kutopata shida wakati wa kusafirisha mali za ujenzi wa kiwanda na kitakapoanza kuzalisha na pia umeme upo karibu.

Kuhusu ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki, Dk. Sengati alitoa wito kwa wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kutoa elimu kwa wafugaji nyuki, ili waweze kuzalisha asali nyingi na iliyobora.

Aliwataka wakazi wa Sikonge na Mkoa wa Tabora kuchangamkia fursa hiyo kwa kujishughulisha na ufugaji nyuki kwa ajili ya maendeleo yao na taifa.

Alisema ili kuwa na maeneo ya kutoa kwa wafugaji nyuki atawasiliana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na mamlaka nyingine za uhifadhi ili waweze kuwa na mahali pa kuweka mazingira bila kubughuziwa.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, Peres Magiri, alisema katika awamu ya kwanza wamepima na kutenga hekta nane kwa ajili ya viwanda vya kati na wako mbioni kupima 200 kwa ajili ya viwanda vikubwa katika awamu ya pili.

Alisema lengo lao ni kutaka kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa viwanda kulingana na uwezo wao na kuwa na maeneo ambayo hayana migogoro.

Awali, Mtakwimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Gadi Mwatebela, alisema walikubaliana na Mfuko wa Misitu Tanzania kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda ambacho kingegharimu Sh. milioni 719.7 na halmashauri kuchangia Sh. milioni 37.8.

Alisema kati ya fedha hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imeshapokea awamu ya kwanza Sh. milioni 462.5 kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kati cha kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki.

Mwatebela alisema ujenzi wa kiwanda hicho uko katika usawa wa lenta na kinatarajiwa kukamilika mwakani.

ama
ALHAMISI DESEMBA 24, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



**Maisha ya ngono na mimba za ajabu visiwa vya Mwanza**

Ukurasa 12



Ukurasa 13

Operesheni tohara inavyosambaratisha Ukimwi ulioshika kasi mkoa Shinyanga



Ukurasa 14

**Mamlaka za Maji zamudu kusambaza, ila mijini yanayopotea njiani tishio**

# Namna ilivyo tatizo la mama anapokosa hedhi kwa wakati

**Na Jackson Paulo**

HALI ya kukosa hedhi kitaalamu inaitwa 'Amenorrhea'. Hiyo inahesabika pale mwanamke anapokosa walau vipindi vitatu mfululizo vya hedhi au binti hajaanza, angalau tayari ana umri wa miaka 15.

Kwa kawaida hedhi huwa mara moja kila mwezi, sababu ya kawaida inayochangia kukosekana hedhi ni ujauzito. Dalili kuu ya shida hiyo ni pamoja na mtu kupata dalili nyinginezo zinazoambatana na kukosa vipindi vya hedhi, ambazo ni pamoja na; utoaji maziwa kwenye chuchu, maumivu ya kichwa, kupoteza kuona vizuri, maumivu ya nyonga, na kutokwa chunusi.

Zipo sababu nyingine zinazochangia kuwa, ni pamoja na tatizo katika mfumo wa uzazi au katika tezi zinazosaidia kudhibiti viwango vya homoni mwilini.



Mwanamke akiwa amelala, akisumbuliwa na tumbo. **PICHA: MTANDAO.**

### UNAMUONAJE DAKTARI?

Mgonjwa anaweza kumuona daktari, kama hajapata angalau vipindi vitatu mfululizo vya hedhi au hajawahi kupata hedhi na tayari umeshafikisha umri wa miaka 15.

Kukosa hedhi kunaweza kuchangiwa na sababu mbalimbali. Baadhi ni za kawaida katika maisha ya mwanamke na kuna wakati inaweza kuwa ni kutokana na athari ya dawa au kiashiria cha tatizo jingine la kiafya. Hapo, sababu zinazochagia kukosekana hedhi na kuna sababnu kadhaa.

Mwanzo, unaanzia katika maisha ya kawaida ya mama, zipo sababu za asili na kawaida zaidi, zinamfanya akose hedhi. Ni pamoja na ujauzito wa mwili, kunyonyesha na ukomo wa hedhi wa asili uitwao kitaalamu 'menopause'.

Pia, katika matazamo wa uzazi wa mpango matumizi ya dawa za uzazi zinaweza kuchangia kukosekana hedhi kwa baadhi ya wanawake.

Hata baada ya kusitisha matumizi ya dawa hizo, bado kuna uwezekano wa kuchukua muda kidogo kwa mzunguko wa hedhi kurejea katika hali ya kawaida.

Tatu, ni matumizi ya baadhi ya dawa zinazomsababisha mwanamke akose vipindi vya hedhi. Kuna baadhi ya dawa zinafanya hedhi kuwa tatizo.

Kuna dawa za magonjwa ya akili, matibabu ya saratani (chemotherapy), dawa za kuzuia mfadhaiko (antidepresants), dawa za kutibu shinikizo la damu, pia za mzio 'allergy'.

Nne, kuna suala la mtindo binafsi wa maisha, kuna wakati humchangia mtu kupata tatizo la hedhi, mathalan uzito wa mwili ulio mdogo kupitiliza huathiri ufanyaji kazi wa homoni, hivyo kusababisha kushindwa kuachiliwa kwa 'yai' kutoka kwenye ovari.

Ni hali ambayo kitalaamu inawafanya kinamama kutopata hedhi. Kinamama ambao wana tatizo la kula, hushindwa kupata vipindi vya hedhi, kwa sababu ya mabadiliko ya homoni yasiyo ya kawaida.

Pia, kuna ufanyaji mazoezi uliopitiliza kwa wanawake wanaoshiriki mafunzo na uwezekano mwingine uko katika msongo wa mawazo, unaoleta mabadiliko kwenye sehemu ya ubongo.

Hata hivyo, vipindi vya kawaida vya hedhi huanza kurejea tena kadri msongo huo unavyopungua.

Lingine ni kuwapo uwiano usio sawa mwilini na unapaswa kuwapo. Ikiwa mwili una tatizo, ni hali inayoweza kuchangia kukosekana hedhi kwa mwanamke. Uwiano wa homoni mwilini unasimamiwa na mengi, ikiwa ni pamoja na kuathirika kwa ufanyaji kazi wa tezi ya kooni na ukomaji mapema wa hedhi ya asili.

Eneo lingine lenye mchango wa athari ni maumbile ya viungo vya uzazi, ambavyo kuna wakati vinachangia mtu kutopata hedhi. Hapo inajumuisha kuwapo kovu katika mji wa kinababa na mwanamama.

Ni hali inayotokea, kuegemea sababu kadhaa kama vile operesheni wakati wa kujifungua (cesarean section) na matibabu ya tatizo la uvimbe kwenye mji wa mimba.

Pia, inawezekana mwanamke anatokea kukosa viungo vya uzazi. Mwanamama anaweza akazaliwa na tatizo la kukosa mfumo wa uzazi kama vile mji wa mimba, kizazi au uke. Iwapo mfumo wa uzazi haupo, ni kawaida hali hiyo kumtokea.

Kunaweza kuwapo nyama nyepesi sehemu ya uke, inayozuia utokaji damu kutoka kwenye mji wa uzazi kuelekea nje.

### HATARI & MADHARA

Hapo inaingia historia ya familia yake, iwapo kuna watangulizi walishapata tatizo la kukosa hedhi, nawanamrithisha.

Tatizo la mlo; ikijumuisha ulafi kupita kiasi au kinyume chake, kula kidogo na kufanya mazoezi magumu. Madhara yanayoweza kuikabili muathirika huyo ni matatizo ya ugumba, kwani mama asiyepata hedhi, hapati ujauzito.

Pia, kuna hatari kiafya ya udhaifu wa mifupa, inayotokana na kiwango kidogo cha homoni aina ya estrojeni, inayosababisha kudhoofika mifupa.

• ***Baruapepe: jacpole@gmail.com***

AFYA

# Maisha ya ngono na mimba za ajabu visiwa vya Mwanza

• Watatu kwa mama, baba tofauti ; hawamjui ndugu zaidi ya mama





Maisha halisi ya makazi ya mwaloni Ilemela na malezi ya watoto waishio huko. **PICHA ZOTE: NEEMA EMMANUEL**

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MALEZI na makuzi bora ya mtoto yanatoka kwa baba na mama, hata akakua katika maadili na kutimiza ndoto sahihi.

Lakini hali ni tofauti katika baadhi ya visiwa, pia katika mialo ya kuvua samaki ya Ziwa Victoria. Kuna wimbi kubwa la watoto wasiowajua baba zao na hawana malezi sahihi.

Inaelezwa mimba nyingi katika ukanda huo zinatumika kushawishi kuolewa, kuimarisha mapenzi na kupata fedha, ambazo kuna sehemu zinaangukia kiza kinene.

Ni simulizi za kinamama kutelekezwa, kutenganishwa na shule, watoto kugeuka vitega uchumi, biashara za ngono, uvuvi, ushushaji samaki na kubebeshwa mimba.

### KWANINI HIVYO?

Nipashe ilifika hapo na kubaini asilimia kubwa ya wakazi Mwalo wa Butuja wilayani Ilemela, uelewa wao kuhusu uzazi wa mpango ni butu mno.

Ally Mkama, Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Butuja, anasema maeneo mengi waliko wavuvi kuna watu wenye vipato vya chini na vipaumbele vyao maishani ni pombe na ngono, hali inayokaribisha mimba zisizotarajiwa.

Mkama anahimiza upekee wa kukemesha hayo kwamba: "Jambo muhimu ni kujikita katika utoaji elimu ya afya ya uzazi, hasa kwa wananchi wa kipato cha chini, kwani ndiko kuna mimba zisizotarajiwa.

"Katika maeneo haya, kuna wakazi wengi na kila siku watu wapya wanaingia, hivyo wengi wanapata ujauzito wakiwa na imani ushawishi wa kuolewa, anafikiria akimzalia mwanae, ndio atampenda lakini mwisho wa siku wanakosa mwelekeo."

> **Elimu ya afya ya uzazi wa mpango nimeipata mara baada ya mwanangu wa pili kuumwa na kupewa rufaa ya kumpeleka Hospitali ya Bugando, ndipo nilishauriwa kutumia njia ya uzazi wa mpango nikijifungua.**

Pia, kuna shuhuda kutoka serikali hiyo ya mtaa, kwamba maeneo mengi yaliyo na mzunguko wa fedha ni wanakopatikana wavuvi, hivyo wanawake na wasichana fukara anarubuniwa kirahisi

"Kuanzia saa 10 jioni hadi 11, utakuta mitumbwi imejazana hapa, utakuta watu wengi wakati mwingine unajiuliza hivi na huyu anafanya biashara ya samaki? " anaeleza Mkama kwa ufafanuzi:

"Ukichunguza unakuta ana jambo lake. Kama jana nilikuwa namwangalia dada mmoja , alikuwa na mtoto mdogo sana ananyonyesha, lakini sasa hivi ana mimba tena ya kujifungua."

Katibu wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi wa Mwambao mwa Ziwa (BMU) ya Mwalo wa Butuja, Emmanuel Nyagwesi, anasema ongezeko la watoto kujifungua kwenye mialo yote na migodi ya dhahabu iko juu.

Anasema, mazingira waliko wavuvi kuna ngono isiyotumia kinga na zinaishia mimba zisizotarajiwa, akiwa na ufafanuzi: "Tunaomba taasisi zinazohusika na masuala ya afya waje watoe elimu kwa jamii hiyo, ili waweze kujua ni namna gani wajikinge na kuzuia mimba zisizotarajiwa."

### MTAALAMU WA AFYA

Bertha Yohana, Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto jijini Mwanza, analalamika penye kundi kubwa la vijana, ndio penye ngono zisizo salama, mimba zisizotarajiwa, utoaji mimba na hata matumizi ya dawa za kulevya.

Mtaalamu huyo wa afya, anaeleza takwimu zinaonyesha wasichana wengi huanza kujihusisha na ngono katika umri wa miaka 18, sawa na asilimia 59 na wavulana miaka 20, sawa na asilimia 45.

"Takwimu zinaendelea kueleza wasichana kati ya umri wa miaka 15 hadi 24 , asilimia 13 waneshajamiiana kwenye umri wa miaka 15 ukilinganisha na asilimia saba kwa wavulana," anaeleza

### WENYE MKASA

Esther (jina la pili tunalo), mama wa miaka 21, mjamzito mwenye watoto wawili; wa kwanza miaka mitatu, wa pili mwaka mmoja, analalamika anaelemewa na kushindwa kuwapatia watoto malezi bora.

Simulizi kuhusu kinachomkabili ni kwamba:

"Nina mimba ambayo karibu nitajifungua, hivyo tabu ninayoipata katika kuwahudumia hawa watoto ni kubwa na huyu wa pili anaumwa mara kwa mara.

"Elimu ya afya ya uzazi wa mpango nimeipata mara baada ya mwanangu wa pili kuumwa na kupewa rufaa ya kumpeleka Hospitali ya Bugando, ndipo nilishauriwa kutumia njia ya uzazi wa mpango nikijifungua."

Rhoda (jina la pili tunalo) , mama anayetetea chanzo kikuu cha maisha hayo yasiyofaa ni shinikizo la dhiki, hata wanafikia kushawishiwa kubeba ujauzito, anasimulia: "Unabeba mimba ukijua huyu atanioa, lakini mwisho wa siku ukimwambia anaikana mimba.

"Anakuambia hiyo ni ya mtu mwingine siyo yake na anaondoka na kuhamia kisiwa kingine, akija mwingine unahisi atakuwa mwema, kumbe ndio 'walewale' hivyo unaamua kuzaa unawapeleka nyumbani au kuwaacha hapa hapa na kuhamia kisiwa kingine."

Japheti Mleka, anayejitambulisha ni mfanyabiashara wa eneo hilo kwa miaka 10 sasa, anaelekeza tatizo kwa wazazi, kwa kuchochea vishawishi watoto kujiingiza kwenye biashara ya ngono.

"Huku wana msemo 'kamoja' kanaitwa 'maelekezo.' Hapa hawatumii mipira ni (kinga), huku ndipo magonjwa yalipo. Pia, ukija muda wa asubuhi au jioni kuna wimbi watoto utawakuta wanaoga ziwani," anasema.

### MABINTI WALIOFIKWA

Stella (jina la pili tunalo) ana umri miaka 16 na wa kwanza katika familia kati ya watatu, anasema alikatisha masomo akiwa darasa la tano, baada ya mama yake kumtaka akafanye kazi kuwapikia wavuvi kisiwa cha Goziba.

Anasema ndiko wavuvi walimfanyia uharamia naye kujihusisha na ngono ikiwamo biashara, kubakwa na alipata mimba aliyoitoa kutumia mitishamba.

"Mwaka huu tu nimetoa mimba, niliumwa sana tumbo na mama alijua. Nilipopona, alinipatia nauli ndio nikaja kwenye mwalo huu. Kwa sasa naishi mwenyewe bila ya mzazi, kwani yeye bado yupo hukohuko.

"Mie simjui baba yangu wala ndugu wa mama yangu na huwa hataki kunipeleka kwao, hivyo leo hii asipokuwapo mama, tutabaki sisi pasipo kumjua ndugu yeyote," anasema na kuongeza uzazi wao watatu wa baba tofauti, wamezaliwa baba tofauti na hakuna anayemfahamu aliyemzaa.

"Bado naendelea kujihusisha na mahusiano, kwa sababu sina kazi yoyote ninayoifanya kuhusu elimu, ningesoma moja kwa moja, ningekuwa kidato cha tatu. Tatizo mama, kila nikifika darasa la tano ananihamisha shule, narudia darasa la kwanza.

"Huwezi amini mwaka huu nilikuwa nasoma darasa la tano kipindi cha corona, ndipo mama alinichukua kwenda Kisiwa cha Goziba, ndipo nilianza kujihusisha na uhusiano na wavuvi," anaeleza.

Dotto (jina la pili tunalo), mwenye miaka 14, baada ya kuhitimu darasa la saba, alianzisha biashara kupika wali na maharage jioni na wateja wake wakuu wavuvi.

"Mimi nina kijiwe changu mtaji alinipatia mama wa Sh. 4000, nimezalisha sasa nina Sh. 25000. Vishawishi ninavyokutana navyo ni vingi, lakini amna namna ninavumilia wakati mwingine mama anakuwapo, ananisaidia kupakua, mie ninahudumia wanaume.

"Ni wasumbufu sana, tena hawa unajua kabisa huyu ana uhusiano na mtu tena sio mmoja, bado anakutaka na wewe, wote hawana malengo zaidi ya kuwachezea mabinti, lakini basi tu huku hamna watoa ushauri na elimu ya kujikinga, " ni kauli ya ulalamishi kutoka kwa Dotto.

Binti huyo anaeleza malengo yake ni kuifikia taaluma ya ukunga, akichukua uhalisia huo ni sehemu ya mapambano.

***. Makala hii ni kwa mujibu wa uchunguzi wa Nipashe.***

AFYA

# Operesheni tohara inavyosambaratisha Ukimwi ulioshika kasi mkoani Shinyanga

• Miaka 9 mambo wameshawagusa, 40%, dira kuu 90% ;Halmashauri Ushetu 'usipime'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKOA wa Shinyanga uko juu katika ushamiri wa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), ukivuka kiwango cha Taifa cha asilimia 5.1, kwani takwimu za mwaka 2011/2012 zilionyesha kuwa na asilimia 7.4.

Hivi sasa kiwango cha kitaifa kiko katika asilimia 4.7 na Shinyanga wastani wake ni juu asilimia 5.9 kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017.

Nini kifanyike? Hadi sasa kunatajwa kuwapo hatua zinazoendelea kukabili kwa wananchi kupima afya kwa makundi maalumu, matunzo na tohara kwa wanaume, huku inahakikishwa kondomu zinapatikana.

Katika kutekeleza mkakati uitwao '95, 95, 95' mkoa unaelekezwa kujipanga kuhakikisha asilimia 95 ya wanaoishi na VVU wanatambua hali zao, kiwango kama pia kinafikiwa kutumia dawa za kufubaza VVU na asilimia 95 zingine wanakuwa na idadi ya virusi vya chini kabisa.

Idadi ya vituo vya kupimaji VVU na ushauri nasaha hadi sasa, vimeongezeka kutoka 137 mwaka 2014 hadi 246 Septemba mwaka huu, huku kwa miezi 11 iloyopita kuna wateja wapya 170,168 waliohudumiwa na kati yao asilimia 4.9 au jumla ya 8452 walionekana na maambukizi ya VVU.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alipozungumza na wananchi wa kijiji na kata ya Mapamba, Halmashauri ya Ushetu, katika maadhimisho Siku ya Ukimwi Duniani, katika kata hiyo mwaka huu. **PICHA: SHABAN NJIA**

### HUDUMA ILIVYO

Tohara imo katika suluhisho la kuengua vijana kuanzia miaka 10 hadi 20 kukabili Ukimwi na kuna mafanikio ya kupungua maambukizi ya VVU kwa zaidi ya asilimia 5.9 katika halmashauri sita za mkoa, Shinyanga, kuanzia mwaka 2010/2011.

Pia, ni hatua inayowanusuru vijana na maambukizi ya VVU na kuwakinga wanawake walioko kwenye ndoa na saratani ya shingo ya mlango wa uzazi kwa kutoa tohara kwa wanaume zao.

Mratibu wa Kudhibiti Ukimwi mkoani, Dk. Peter Mllacha, anadai Halmashauri ya Msalala, inaongoza kwa kutoa huduma ya tohara baada ya vijana na watu wazima 110,007 kujitokeza kupata huduma hiyo.

Katika Halmashauri ya Kahama Mjini walijitokeza 85,940; Kishapu 48,837; Shinyanga Vijijini 69,820; Manispaa Shinyanga, 39,431; na Halmashauri ya Ushetu 106,332. Kwa ujumla, vijana na watu wazima walifanyiwa tohara ni 460,367.

### MRATIBU UKIMWI

Dk. Peter Mllacha, Mratibu wa Kudhibiti Ukimwi Mkoa wa Shinyanga, anasema huduma ya tohara kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 10, ndio kioo cha kufanikisha kupungua Ukimwi hadi asilimia 5.9 kutoka zaidi ya asilimia saba za awali.

> "Unapofanyiwa tohara unajikinga na VVU kwa asilimia 60 na unakuwa unamkinga mwenza wako na saratani ya shingo ya mlango wa uzazi.

Anasema, kwa miaka tisa waliendesha huduma hiyo kwa mafanikio kufikia asilimia 40 ya vijana na watu wazima mkoani, dira iliyoko ni kuifikia asilimia 90 ya kundi hilo na utafiti wa kimkoa unaonyesha VVU imepungua kwa asilimia 60.

Dk. Mllacha anasema, kundi hilo linatajwa ndilo kwa kiasi kikubwa limejitokeza kwa hamasa kufanyiwa tohara, wakilinganisha na wenye umri mkubwa zaidi, kazi iliyofanyika kupitia Ofisi za Watendaji wa Kata, zilizofanyiwa maboresho.

"Unapofanyiwa tohara unajikinga na VVU kwa asilimia 60 na unakuwa unamkinga mwenza wako na saratani ya shingo ya mlango wa uzazi.

"Hivyo, vijana na watu wazima ambao bado hawajafanyiwa huduma hii, wajitokeze kwenye vituo vilivyopo jirani yao na kupata huduma," anasema Dk. Mllacha.

### SHIDA KUU ZILIZOPO

Anasema juhudi za mkoa kupambana na kuenea Ukimwi, wapo wanaotambulika kuwa na maambukizi ya VVU wanaoacha kuchukua dawa za kufubaza au wanahama, pasipo kutoa taarifa za mahali walikoenda.

Pia, analalamika kwamba idadi ya Vituo vya Huduma na Matunzo (CTC) havitoshi, ikilinganishwa na wananchi waliopo na kwa mujibu wa mratibu huyo, kuna vituo 85 tu vinavyotoa huduma hiyo, kati ya 246 zilivyopo sawa na asilimia 34.5 ya mahitaji halisi.

Dk. Mllacha anawalalamikia wanaume kuwa na ushiriki mdogo wa wanaume katika kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, huku kukiwapo wanaoanzishwa dawa za kufubaza VVU au ARV, wanaacha kiholela.

Kwa mujibu wa Mratibu Ukimwi, kuna wagonjwa 4,516 waliokuwa wanatumia ARV walitoweka, ila juhudi zilifanyika na kuwarejesha 3,016 walioendelea nazo.

### MRATIBU WA TOHARA

Haji Sued, ni Mratibu wa Huduma za Tohara katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, anasema wamefanikisha kupunguza wimbi la maambukizi kwa asilimia 5.3 kutoka asilimia 6.4 za awali.

Pia, anataja pia ushindi katika kupunguza ugonjwa wa saratani ya shingo ya uzazi kwa kinamama kwenye ndoa na wajawazito wanaelimishwa kliniki, umuhimu wa tohara kwa wenza.

"Kumeibuka uzushi mitaani kwamba tohara inapunguza nguvu za kiume jambo ambalo halina ukweli kabisa...tohara haipunguzi nguvu za kiume na haiongezi nguvu za kiume wala kuongeza ladha ya mapenzi au kupunguza, ila inamkinga mtu kutopata maambukizi ya Ukimwi," anasema Sued.

Msimamizi wa Kitengo cha Tohara katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Damson Samweli, anasema mwaka huu na ujao, wanatarajia kutoa huduma hiyo kwa vijana wa miaka 15 na kuendelea zaidi ya 14,000 wa Kahama.

Anasema, kati ya Oktoba ya jana na mwaka huu, walitarajia kuwafikia zaidi ya vijana 6,755 kwa huduma ya tohara.

### VIONGOZI SERIKALINI

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu (DMO) Dk. Senguo Nicodemus, anasema tohara imewapunguzia Ushetu, maambukizi ya VVU kwa asilimia tatu nao wanaendelea kutoa elimu kwa makundi ya vijana wajitokeze kwa hiari.

Anatoa takwimu ya Januari hadi Novemba mwaka huu walipima virusi VVU kwa zaidi ya wananchi 32,000 na waliokutwa na athari wote waliandikishwa na kuanzishiwa dawa mara moja kwenye vituo jirani yao na rai yake, mke na mwenza kupima afya kwa, pindi wanapopata huduma hospitalini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Ushetu, Michael Matomora, anasema wananchi wa kata hiyo wanapata changamoto ya kukosa kituo cha tiba na matunzo kwa wanaoishi na VVU, hata kusababisha kutembea umbali wa kilomita nane hadi 10 kwenda Kituo cha Afya Ukune. Pia, anataja zahanati za Busenda, Uyogo na Chambo.

Katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Mkoa wa Shinyanga yaliyofanyika katika Kata ya Mapamba, katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, kulibainika huduma ipatikanayo katikia Kituo cha Tiba na Matunzo kwa Wanaoishi na VVU, kuna changamoto kubwa.

Ni hali iliyosababisha kuchukuliwe hatua ya papo kwa hapo, kuchangwa jumla Sh. milioni 6.8, kusaidia kujengwa kituo hicho.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, katika maadhimisho hayo, anasema lengo la kujenga kituo hicho ni kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mwananchi, Abel Maziku, anasema licha ya kata kuwa na zahanati bado wananchi wanalazimika kutembea umbali huo wa kilomita nane hadi 10 kusaka tiba.

MAZINGIRA

EWURA YAANIKA...

# Mamlaka Maji zamudu kusambaza, ila mijini yanayopotea njiani tishio

• Zinazopotea 40%; kitaifa wafikiwa nusu • Mbivu na mbichi za ripoti mpya mbioni



Rais John Magufuli, alipozindua mradi wa maji mkoani Arusha. **PICHA: MTANDAO**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MATATIZO makubwa na kuibuka mahitaji ya maji kwa umma, serikali imekuwa ikivalia njuga hitaji hilo, kuhakikisha huduma yake inaboreshwa zaidi.

Hiyo inajumuisha kuongezwa bajeti, kuanzishwa na kuimarishwa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira ili kuboredha huduma hiyo muhimu.

Mwanzoni mwa miaka ya 2000 serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), lengo ni kuhakikisha huduma husika inatolewa kwa ubora na viwango vya juu.

Licha ya juhudi hizo, hali ya utoaji wa huduma za maji ilikuwa haikuwa ya kuridhisha sana katika baadhi ya maeneo, ikiwamo miji mikuu ya mikoa na wilaya, ambako kuna mamlaka hizo za maji.

**NINI KINAFANYIKA?**

Hivi sasa EWURA inaandaa Ripoti ya Mapitio ya Utendaji wa Huduma za Maji kwa wilaya na miji kwa mwaka 2019/20, inayotarajiwa kuwa na uchambuzi linganishi wa kiwango cha utendaji wa huduma za maji za wilaya na miji 94, mikoa 26 na miradi ya kitaifa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, anasema kupitia vielelezi vya mkutano wao, itaandaliwa ripoti kutathmini utendaji wa kila shirika la maji viwango vyao vya huduma za maji safi na usafi wa mazingira.

> **"Mwanzoni mwa miaka ya 2000 serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), lengo ni kuhakikisha huduma husika inatolewa kwa ubora na viwango vya juu.**

Anasema Sheria ya Usambazaji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019, mamlaka ya maji ina jukumu la kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira, licha ya umakini kuelekezwa zaidi katika huduma za maji zaidi.

Chibulunje anasema: "Kwa hiyo, mamlaka hizo zinahitajika kuhakikisha kuwa zinakusanya na kuwasilisha taarifa na habari juu ya hali ya usafi wa mazingira katika maeneo yao ya huduma kama ilivyokuwa ikiwasilishwa na EWURA hapo awali.

"Matokeo yatakayoainishwa katika ripoti hii yatakuwa kumbukumbu kuu kwa Bodi za Wakurugenzi na Usimamizi wa Huduma za Maji za Wilaya na Miji, ili kuboresha huduma ya maji na huduma za usafi wa mazingira katika maeneo yao ya huduma."

Kaimu Mkurugenzi huyo anasema, ripoti hiyo itakuwa nyenzo muhimu kutathmini maendeleo kuelekea kufikia Malengo ya Kitaifa na Kimataifa ya utoaji Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira.

Chibulunje anawataka wadau hao wa mamlaka za maji kuhakikisha wanatoa taarifa sahihi na habari kwa ajili ya kuandaa ripoti, akiwakumbusha mahitaji ya kuripoti kama ilivyoainishwa katika Leseni ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira 2020 (Leseni naUbora wa Sheria za Huduma).

**RIPOTI ILIYOPITA**

Katika Ripoti za Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini mwaka 2017/18 iliyotolewa na EWURA, ilichambua utendaji wa mamlaka 82 zinazojumuishwa na 68 za miji mikuu ya wilaya na 14 za miji midogo.

Hapo ilionyesha jumla ya mamlaka 15 hazikufanyiwa tathmini kutokana na kutowasilisha taarifa za utendaji na mamlaka 13, zilikuwa hazijaanza kutoa huduma kwa kuwa hazikuwa na menejimenti na bodi ya wakurugenzi.

Aidha, tathmini ya utendaji wa Mamlaka zinazohudumia miji mikuu ya mikoa na miradi ya kitaifa, inaonyesha utendaji wa mamlaka umeimarika katika nyanja mbalimbali.

Hapo kunatajwa kuongezeka kwa kiwango cha maji kinachozalishwa na wanaoafikiwa na huduma, ubora wa maji, wateja wake na wa mtandao wa majitaka.

Pia, ripoti inataja wastani wa muda wa upatikanaji maji kwa siku, kuimarika uwiano wa wafanyakazi na idadi ya wateja, makusanyo yatokanayo na malipo na idadi ya mamlaka za maji za mikoa zinazofanya vizuri, kwa mujibu wa vigezo vya EWURA.

Vilevile, ripoti inaonyesha utendaji wa mamlaka zinazohudumia miji ya makao makuu ya wilaya na miji midogo, umeimarika.

Hata hivyo, ripoti inadokeza na sura ya pili katika hatua hiyo ya maendeleo, kuwapo vikwazo vingi vinavyohitaji ufumbuzi mpana.

**MIRADI KITAIFA**

Maji yanayozalishwa na miradi ya kitaifa yanatajwa yamepungua kwa asilimia tatu na kwamba inatokana miradi minne ya kitaifa ambayo ni Maswa: Makonde, Mugango Kiabakari na Manawasa.

Kiwango kilichozalishwa nusu ya mahitaji, yaani asilimia 51.2 katika maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa kwa mwaka 2017/18 na muda wa upatikanaji wa maji hayo umekuwa wastani wa saa 14 kwa siku.

Vilevile, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira za miji ya makao makuu ya mikoa zilikuwa na ongezeko la asilimia 9.2 na kiwango cha ufungaji dira za maji za wateja kiliongezeka kwa hatua kubwa.

Pia, ufanisi wa kukusanya mapato ya maii huko mikoani imefika hadi asilimia 93.6 kwa mwaka wa fedha 2017/18 na miradi ya kitaifa ikivuka lengo hadi asilimia102.5 kwa mwaka huo wa fedha, kutoka asilimia 75.6 mwaka uliotangulia.

Ripoti hiyo inaainisha mamlaka zinapaswa kuongeza jitihada za kuhakikisha wateja wote wanafungiwa mita za maji, ili kudhibiti upotevu wa maji na kuongeza mapato ya mamlaka zao.

**UPOTEVU WAKE**

Mafanikio hayo katika utoaji huduma za maji nchini, yanakazwa na kiwango kikubwa cha maji kinachopotea njiani kwa mamlaka za maji za miji mikuu na mikoa, kimeongezeka toka asilimia 38.4 mwaka wa fedha 2016/17 hadi asilimia 40.5 kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Hata hivyo ni kinyume chake kwa mamlaka za maji za miradi ya kitaifa, kwani katika kipindi hicho kiwango cha upotevu wa maji kimepungua kutoka asilimia 33.1 hadi asilimia 26.8.

Aidha, inaelezwa, uzalishaji maji ni wastani wa asilimia 67.9 tu ya mahitaji katika miji ya makao makuu ya mikoa na mtandao wa usambazaji majisafi unakidhi asilimia 74 kwenye miji ya makao makuu ya mikoa na asilimia 55 miradi ya kitaifa.

Akizindua ripoti hiyo, aliyekuwa Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa, aliitaka EWURA kuzilea na kusimamia mamlaka za maji zidhibiti upotevu wa maji uliopanda hadi kufikia asilimia 40.5 kutoka asilimia 38.4.

Agizo lake ni kwamba EWURA izilee na kuzisimamia mamlaka hizo, ziweze kuzalisha maji na kuhakikisha mahitaji hayo yanawafikia wananchi walengwa.



# Aweso aipa kibarua Bodi RUWASA

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameitaka Bodi ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) na menejimenti yake kuhakikisha ifikapo Machi, mwakani, iwe imekamilisha miradi ya maji yenye matatizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliitolewa na Kitengo cha Mawasiliano cha Wizara ya Maji, Aweso aliiagiza RUWASA kuainisha miradi yote ya maji vijijini yenye matatizo, zikiwamo gharama zake na namna ya kuzitatua.

Maagizo hayo aliyatoa katika kikao kazi na wajumbe wa Bodi ya RUWASA na menejimenti, kilichofanyika jijini hapa kwa lengo la kuimarisha sekta ya maji itakayosaidia wananchi kupata maji yanayojitosheleza.

Waziri Aweso alisema hadi Machi, mwakani, miradi yote inapaswa kuwa imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake, ili kuhakikisha wananchi wanapata majisafi, salama na yanayojitosheleza katika maeneo husika.

“Hakikisheni mnafanya kazi kwa ushirikiano na timu moja ya wizara, ili kutimiza lengo letu la kuwahudumia wananchi na kuwapatia majisafi na ya kutosheleza,” alisema Aweso.

Pia alisema RUWASA inapaswa kuimarisha ushirikiano na Chuo cha Maji kwa kuwatumia wataalamu wanaotoka katika chuo hicho kwenye usimamizi wa miradi inayotekelezwa jambo ambalo litasaidia kuongeza nguvu ya utendaji kazi.

Waziri huyo alisisitiza RUWASA kubainisha miradi yote iliyokamilika kwa kutumia wataalamu wa ndani ‘force account’ na miradi hiyo inapaswa kuwa endelevu kwa kuunda vyombo vya watumia maji wenye uwezo wa kusimamia na kuendesha miradi hiyo kikamilifu.

Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Clement Kivegalo, alisema moja ya changamoto inayowakabili ni rasilimali watu na bado wanahitaji wataalamu ili kujiimarisha zaidi kiutendaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya RUWASA, Prof. Idrissa Mshoro, aliishukuru serikali kwa kuwawezesha katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha miradi ya maji vijijini inakamilika.

Prof. Mshoro alisema bodi hiyo imeielekeza RUWASA kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ili kuhakikisha wananchi wanapata maji ipasavyo.



Mchuuzi Renard Mbelele akisaka wateja wa miti ya mapambo kwa ajili ya sikukuu ya Krismasi eneo la soko la Majengo, jijini Dodoma jana, kila mti uliuzwa kwa Sh. 3,000 hadi Sh. 2,500. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Waziri wa Kilimo aomba ushirikiano

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amewataka watumishi wa wizara hiyo kutoa ushirikiano katika utendaji kazi, ili kuongeza tija kwenye mazao.

Prof. Mkenda ambaye alifuatana na Naibu Waziri wake, Hussein Bashe, walipokewa rasmi juzi na menejimenti ya wizara katika ofisi zilizoko Mji wa Serikali Mtumba, jijini hapa.

Katika mazungumzo yake na menejimenti ya wizara pamoja na wakuu wa taasisi, Prof. Mkenda alisema ili kuongeza tija kwenye sekta ya kilimo, mazao hususan ngano na mengine ya biashara ushirikiano unahitajika.

Katika hafla hiyo ya mapokezi, wote kwa pamoja walipata nafasi ya kuzungumza, huku Mkenda akisisitiza kuwa wizara ina jukumu kubwa la kuhakikisha taifa linaendelea kujitosheleza kwa chakula na kufanya sekta ya kilimo kuchangia maradufu katika pato la taifa. Waziri Mkenda aliongeza kuwa tija kwenye kilimo bado iko chini na mazao yanachangia asilimia 18 ya pato la taifa wakati sekta ya kilimo kwa ujumla inachangia takribani asilimia 28.2 ya pato la taifa, asilimia 58 ya ajira na asilimia 65.5 ya malighafi inayotumika katika viwanda, asilimia 28.2 ya pato la taifa na asilimia 30 ya mapato ya fedha za kigeni.

“Ukitazama zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wameajiriwa kwenye sekta ya kilimo. Jambo hili ni lazima tulifanyie kazi kwa ukaribu na kuleta mapinduzi ya kweli,” alisema. “Nchi zilizoendelea unakuta asilimia tano tu ndiyo wameajiriwa maana yake ni kuwa tija iko chini. Unatakiwa kuwa na idadi ndogo na wengine wajikite kwenye sekta zingine,” alisema.

Naibu Waziri Bashe alisema ili wizara ifikie malengo yalikusudiwa ni vyema viongozi na watumishi wote wa wizara wakabadili fikra. Alisema kwa kufanya hivyo, kila kitu kitabadilika ikiwamo utendaji kazi wa kila siku.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, kwa niaba ya watumishi wa wizara, aliahidi kutoa ushirikiano kwa viongozi hao wakuu wa wizara ili watekeleze majukumu yao.

# Ummy ataka miti mil. 1.5 kila mwaka

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Ummy Mwalimu, ameziagiza halmashauri zote nchini kupanda miti 1,500,000 kila mwaka ili kuhifadhi mazingira kwa vizazi vijavyo.

Agizo hilo alilitoa wakati wa uzinduzi wa jiwe la utambulisho wa eneo la mfano wa msitu lililoko Medeli, alipokuwa akizungumza na wananchi na wadau wa upandaji miti na utunzaji wa mazingira jijini hapa.

Waziri Ummy alisema halmashauri zote nchini zinawajibika kupanda idadi hiyo ambayo itasaidia kupunguza ongezeko la joto.

“Agizo langu kwenu ninyi maofisa misitu wa halmashauri zote hapa nchini, mhakikishe mnapanda hiyo idadi ya miti kila mwaka ambayo itakuwa faida kwa vizazi vijavyo na pia kupunguza joto,” alisisitiza.

Mtaalamu wa Mazingira kutoka Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF), Dk. Severin Kalonga, alisema miche 40,000 imepandwa katika eneo la msitu wa Medeli na asilimia 90 ya miche hiyo imepona.

“Hapa tulipo waziri sisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tumepanda zaidi ya miche 40,000 na kwa asilimia kubwa miti yote imestawi kama unavyoiona kwenye eneo hili la mfano,” alisema.

Naye Zureikha Kachwamba, Ofisa Misitu kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) alibainisha kuwa miti 1,400,000 imepandwa katika Jiji la Dodoma na miche 500,000 iko katika bustani na inatarajiwa kupandwa.

Katika hatua nyingine, Ofisa Mazingira Mkoa wa Dodoma, Salvatory Mashamba, aliomba jamii inapopanda miti kuhakikisha inakuwa kwa kuzingatia sheria ya jiji ya upandaji wa miti mitano kwa kila familia.

Mradi wa kukijanisha Dodoma unasimamiwa na Vodacom Foundation kwa kushirikiana na serikali, WWF na TFS.



## Wataka elimu ya kilimo hai

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wameiomba serikali kupitia maofisa kilimo kupeleka elimu ya kilimo hai maeneo ya vijijini, ili kuepuka matumizi ya mbinu za kilimo zinazochangia uharibifu wa mazingira.

Walitoa ombi hilo juzi, wakati wa mafunzo ya kilimo hai kwenye Chuo cha Kilimo Uyole cha jijini hapa ambayo yalitolewa kwa ushirikiano na Taasisi ya Kilimo Hai (SAT) ya mkoani Morogoro.

Mmoja wa wakulima hao, Mosea Mwaigomole, kutoka katika kijiji cha Ndaga wilayani Rungwe, alisema baada ya kupata mafunzo hayo, walibaini mbinu hizo walizofundishwa ni nzuri na zinafaa kufundishwa kwa wakulima wengi.

Alisema maeneo mengi ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ardhi yake imechoka kutokana na matumizi ya mbinu za kilimo ambazo zimekuwa zikichangia uharibifu huo wa mazingira.

"Tumeambiwa kwamba mbinu hizi za kilimo hai zinasaidia kutunza rutuba kwenye udongo pamoja na kuepusha mmomonyoko wa udongo, sasa ukiangalia kwenye maeneo yetu mengi tumesharibu udongo," alisema Mwaigomole.

Naye Prisca John, alisema kwa mujibu wa elimu waliyoipata kuhusu kilimo hicho ni kwamba kinasaidia kupunguza gharama za uzalishaji kutokana na kwamba mbolea za kisasa hazitumiki kwa kiasi kikubwa. Alisema endapo wakulima wengi zaidi watahamasika kuzitumia mbinu hizo kuna uwezekano hata uzalishaji ukaongezeka katika mikoa hiyo pamoja na kulinda afya ya udongo.

Mwezeshaji kutoka SAT, Hugo Kunguru, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji bila kuharibu rutuba ya udongo kwenye mashamba yao.

Alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula, lakini hata kiwango cha uharibifu wa afya ya udongo kipo juu.

# RC ataka Magereza kuanzisha kiwanda cha kuchakata mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amelitaka Jeshi la Mgereza mkoani hapo, kuanzisha kiwanda cha kuchakata mazao ya nafaka hasa mahindi ili kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa.

Chalamila alitoa ushauri huo juzi, alipofanya ziara katika Gereza la Kilimo la Songwe mkoani hapa kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli la kuhakikisha jeshi hilo linaongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula.

Alisema moja kati ya viwanda ambavyo jeshi hilo linatakiwa kufikiria ni kiwanda cha kuzalisha unga na vyakula vya mifugo vinavyotokana na mahindi ambayo linazalisha lenyewe ili badala ya kusafirisha mahindi ghafi lisafirishe bidhaa zilizochakatwa.

Lengo kuu la serikali, kwa mujibu wa Chalamila, ni kuhakikisha Magereza inajitosheleza kwa chakula cha wafungwa badala ya kutegemea bajeti kutoka serikali kuu, ili fedha hizo zitumike kwa ajili ya shughuli zingine za maendeleo.

"Mkifanya hivyo mtakuwa mmeongeza ufanisi katika uendeshaji wa magereza yetu. Wafungwa watakula vizuri kwa sababu chakula kipo maana hawa ndio wanaofanya hii kazi ya uzalishaji. Lakini mtapata fedha kwa kuuza baadhi ya vitu mnavyozalisha," alisema Chalamila.

Alisema gereza hilo ni moja ya magereza ambayo yanategemewa nchini kwa uzalishaji wa chakula. Alisema hivi karibuni zaidi ya tani 200 za mahindi zilisafirishwa kwenda katika mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro kutoka kwenye gereza hilo.

Katika ziara hiyo, Chalamila alizungumza na wafungwa wa gereza hilo na kuwataka kufanya kazi kwa bidii kwa kuwa kazi wanazofanya ni sehemu ya mafunzo ya kuwabadili tabia ambazo walishindwa kuzifanya uraiani.

Alisema lengo la serikali kuwaweka wahalifu gerezani si kuwatesa bali ni moja ya maeneo ya usalama wao kwa kuwa kuna uwezekano wangekuwa uraiani wangekuwa walishauawa na wananchi wenye hasira kutokana na matukio yao.

"Ninyi mnatakiwa kujitosheleza kwa chakula. Fanyeni kazi kwa bidii, endapo chakula kitakosekana, ninyi mtakufa kwa njaa, sasa kuletwa gerezani haimaanishi ufe," alisema Chalamila.

Mkuu wa Magereza wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Mathias Mkama, alisema wameongeza maeneo ya kulima kwa kuongeza ekari 500 ambazo wamelima mahindi ya kumwagilia.

Alisema wanawatumia wafungwa kufanya shughuli hizo na baadhi ya maeneo wanayolima wanatumia matrekta ambayo walipatiwa na serikali kwa ajili ya kufanyia kazi.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (mbele), akitoa maelekezo kwa maofisa wa Jeshi la Magereza alipotembelea mashamba ya Gereza la Kilimo la Songwe juzi, ili kuangalia utekelezaji wa maelekezo ya serikali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Marufuku disko toto Krismasi, Mwaka Mpya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KUELEKEA Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, limepiga marufuku kumbi za starehe kuandaa mziki kwa ajili ya watoto, maarufu kwa jina la 'Disco Toto' kwa kuwa mazingira hayo siyo salama kwa kundi hilo.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alipiga marufuku hiyo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu jeshi hilo, lilivyojipanga kulinda usalama wa raia na mali zao.

Aliwataka wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuendelea kuzingatia ulinzi wa mtoto kwa kuwaepusha na mazingira yasiyo salama kwao ikiwamo kumbi za starehe na matembezi yasiyo ya lazima.

"Lakini pia tunawataka wazazi na walezi kuwaepusha watoto na matembezi au safari na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima, ili kuepuka watoto kupotea katika msimu huu wa sikukuu," alisema Kamanda Matei.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanaimarisha ulinzi na usalama kwenye makazi yao ikiwamo kuacha mtu angalau mmoja nyumbani wanapokwenda makanisani au kwenye mikesha ya aina yoyote ili kuepuka wezi kuitumia nafasi hiyo kuiba.

Pia aliwataka viongozi wa serikali ngazi ya mitaa, vijiji na kata kushirikiana na Polisi Kata walioko kwenye maeneo yao ili kuimarisha ulinzi na usalama.

Alisema jeshi hilo litahakikisha sherehe zote za mwisho wa mwaka na zingine zitakazofanyika mwakani zinafanyika kwa amani na utulivu katika maeneo yote.

Aliwasisitiza viongozi wa makanisa mbalimbali kuweka utaratibu mzuri wa ulinzi kwa kutumia Kamati za Ulinzi na Usalama zilizopo, ili kuhakikisha hali ya utulivu inakuwapo nje na ndani ya nyumba za ibada.

Matei alisema jeshi hilo litahakikisha linaimarisha ulinzi kwenye mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela, ili kuzuia uingizwaji wa bidhaa za magendo kupitia njia za panya hasa kutoka katika nchi jirani ya Malawi.

"Tumejipanga vyema kuhakikisha watumiaji wa vyombo vya moto na watumiaji wengine wa barabara wanatii sheria za usalama barabarani katika maeneo yote ya mkoa huu. Yeyote atakayekamatwa kwa kukiuka sheria atashughulikiwa ipasavyo," alisema Kamanda Matei.

Alisema moja ya vitu ambavyo watahakikisha wanadhibiti ni pamoja na madereva wa vyombo vya moto kuendesha, huku wakiwa wamelewa au kwa mwendo kasi ambao utahatarisha maisha yao na ya watumiaji wengine wa barabara.

Jeshi hilo, alisema litaendelea kusimamia utaratibu wa magari ya abiria na ya mizigo kupita kwa awamu katika maeneo ya miteremko mikali ukiwamo wa Iwambi, Mwansekwa, Mlima Nyoka na Igawilo na eneo la Uwanja wa Ndege wilayani Rungwe.

Alisisitiza kuwa jeshi litaimarisha ulinzi katika maeneo muhimu ikiwamo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA) na katika fukwe za Ziwa Nyasa wilayani Kyela.





Meli ya Mv Mbeya ikiwa imetia nanga katika Bandari ya Mbamba Bay wakati wa tamasha la utalii lililofanyika hivi karibuni mkoani Ruvuma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atangazia kibano walioficha mafuta ya kula

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imetoa mwezi mmoja kwa wafanyabiashara ambao wameficha mafuta ya kupikia kuyatoa na kuyauza kwa wananchi kwa bei ya kawaida.

Kaimu Waziri wa Wizara hiyo, Mudrik Ramadhan Soraga, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari Mwanakwerekwe, kutokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta hayo ambayo sasa yanauzwa Sh. 58,000 kwa dumu la lita 20 badala ya Sh. 48,000.

Alisema kumekuwapo na wafanyabiashara wakiwa wanategea kwa makusudi na kuyaficha mafuta hayo, ili wakiona yametetereka wanayatoa na kuyauza kwa bei ya juu.

Mudrik alisema atahakikisha akiba ambayo wanayo ya mafuta inatoka na kuingia sokoni na kwamba iwapo agizo hilo halitotekelezwa, serikali itatoa bei elekezi.

Awali, alisema kulijitokeza changamoto ya kupanda kwa mafuta hayo, lakini hivi sasa mafuta yapo ya kutosha na kuwataka wananchi wasiwe na wasiwasi juu ya bidhaa hiyo.

"Tamko la wizara kwamba wafanyabiashara ambayo mafuta wanayo na kama walinunua kwa bei ya zamani wasiyauze kwa bei ambayo ipo sasa hivi," alisema.

"Hivi karibuni tulipokea changamoto ya soko la mafuta ya kupikia kutoka kwa wananchi na kwa baadhi ya vyombo vya habari kwamba bei ya mafuta imeongezeka kutoka Sh. 48,000 hadi Sh. 58,000," aliongeza.

Waziri alisema hali ya soko la mafuta kwa Zanzibar kwa sasa ni nzuri na kwamba kuna akiba ya zaidi ya tani 2,430 na wastani wao wa matumizi kwa mwezi ni tani 418, hivyo wana akiba ya zaidi ya miezi sita.

Hata hivyo, alisema sababu kubwa ambayo ilifanya mafuta hayo kuongezeka kwa bei ni kutokana na kupanda kwa bei katika soko la dunia ambako dumu la lita 20 linauzwa kati ya dola 20 na 25 na uingizaji wa ndani ni Sh. 55,000 mpaka Sh. 58,0000.

Aliitaja sababu nyingine ya kuongezeka kwa bei kubadilika kwa soko la dunia, lakini kuna mahitaji makubwa ya mafuta nchini China ambao wanahitaji tani milioni 1.7 mpaka kufikia mwaka 2023 na hali iliyosababisha meli nyingi kusafirisha mafuta huko.

Hata hivyo, alisema kuna matarajio makubwa ya kupungua kwa mafuta katika kipindi cha miezi michache ijayo huku idara ya biashara ikifuatilia kwa karibu taarifa ya ziada ili kuingia katika mfumo sahihi na kupata bei zinazostahili.

# Wakurugenzi mabaraza miji watumbuliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, amewatumbua wakurugenzi wawili wa mabaraza ya mji Zanzibar.

Wakurugenzi hao ni wa Manispaa ya Mjini, Said Juma Ahmada, na wa Baraza la Manispaa Magharibi 'A', Amour Ali Mussa, kutokana na tuhuma mbalimbali zinazowakabili ikiwamo ubadhirifu wa fedha za umma.

Pamoja na kuwatumbua, waziri huyo ameagiza kuanza kufanyika kwa uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili wakurugenzi hao na nafasi zako kukaimiwa na watu wengine kwa mujibu wa sheria.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisi kwake, Vuga mjini Unguja, waziri huyo alisema uamuzi huo umekuja baada ya kukamilika kwa ziara yake katika taasisi mbalimbali zilikuwa chini ya wizara yake.

Alisema katika ziara hiyo, amebaini uwapo wa ubadhirifu wa mali za umma, urasimu, rushwa na kutowajibika kwa baadhi ya watendaji wa manispaa, halmashauri na mabaraza ya miji.

Pia waziri huyo alimwagiza Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kuivunja bodi ya zabuni ya JKU, ili kupisha uchunguzi na hatua mbalimbali za kisheria kuchukuliwa.

Pia aliagiza wakuu wote wa idara maalum za SMZ kufanya uhakiki wa watumishi wote kuagiza kuanzia mwakani, mishahara ya watumishi wa idara hiyo ilipwe taslimu badala ya benki kutokana na uwapo kwa viashiria vya watendaji hewa.

Katika hatua nyingine, Masoud aliwaagiza wakuu wa mikoa ya Unguja na Pemba kutathmini upya uwezo wa utendaji kazi wa masheha wote na kamati zao za shehia na endapo watabaini kuna udhaifu wa aina yoyote watengue uteuzi wao.

## Makamu wa Rais akunjua makucha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amemwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, kumsimamisha kazi mara moja ofisa wa Idara ya Ustawi wa Jamii anayehusika na utoaji wa kibali kwa ajili ya uendeshaji wa huduma za watoto yatima kwa kudharau wito.

Hemed alitoa agizo hilo jana, alipofanya ziara fupi ya kukagua mradi wa ujenzi wa majengo ya watoto yatima katika mtaa wa Jumbi, Wilaya ya Kati Unguja na kutokukuta ofisa yoyote wa idara hiyo katika eneo hilo licha ya kupewa taarifa ya ziara hiyo.

Alisema hicho ni kitendo cha dharau kilichoonyeshwa na mtumishi huyo wa idara ya ustawi wa jamii kwa vile hadi inamalizika ziara hiyo, hakuna sababu zozote zilizowasilishwa kwa kutokuwapo kwake katika wito huo wa mtendaji mkuu huyo wa shughuli za serikali.

Hemed alisema haiwezekani kuona baadhi ya watu, hasa watumishi wa umma, wanaendelea kwenda katika mfumo wa mazoea wakati taasisi, jumuiya na hata baadhi ya mashirika ya kiraia zimeshajitolea kusaidia nguvu katika uwezeshaji wa hifadhi ya watoto walioondokewa na wazazi wao.

Makamu wa Pili huyo alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kufuatilia suala la ucheleweshwaji wa upatikanaji wa kibali kwa ajili ya uendeshaji wa huduma za yatima katika majengo hayo.

Pamoja na kuagiza kufuatiliwa, alisema lazima kipatikane mara moja ili huduma hizo zianze kwa wakati.

Akizungumza na wasimamizi wa mradi wa ujenzi huo baada ya kuutembelea, Hemed alisema watumishi watakaopewa jumuku la kuwahudumia watoto yatima lazima wawe makini na kuwa macho kwa kuwaepusha watoto hao na wimbi la vitendo vya udhalilishaji.

Hemed alisema watoto yatima wanahitaji matunzo mazuri na uangalizi mkubwa utakaowapa faraja ya kujihisi kama wenzao mfumo utakaohitaji kwenda sambamba na haki zao zote katika mazingira ya kimaisha.

Alisisitiza umuhimu wa kuzingatia mazingira bora ya usafi ndani ya majengo hayo ili watoto wote waendelee kuishi kwa amani, afya na upendo miongoni mwao na walezi wao.

Naye Msimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Majengo hayo, Mohammed Mansour, alisema makazi hayo yatahudumia watoto yatima 15.

Alisema ujenzi huo umezingatia zaidi suala la upatikanaji wa huduma za maji safi na salama zilizopelekea kuchimbwa kwa kisima maalum katika eneo hilo, ili kuondoa usumbufu wa huduma hiyo muhimu kwa jamii.

Naye Zainab Ali Kutoka ubalozi wa Kuwait, alisema uongozi wa kituo hicho umezingatia kwa kina watu watakaoajiriwa katika kazi hiyo tayari wana uzoefu wa kina katika huduma za usimamizi wa malezi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

**Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.**


## OFISI ZA MATANGAZO

Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com


## KUPOTEA KWA VYETI



**FATUMA MUSSA KAMKUMBA** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba **S0831/008** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **NANGWANDA GIRLS mwaka 2014** na cheti cha chuo index namba NA/24615/M3 mwaka 2016,yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa**
**MTW/NEW/RB/866181/2020**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo:**
**MJINI MOROGORO.**

Usimamizi wa mirathi No; 376/2020

Ombi la STEPHEN AMBROSE MKOBA, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AMBROSE E.MKOBA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/01/2021 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/12/2020.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**
**Wilaya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 247/2020**
**MDAI KEPHAS SHABAN**
**MDAIWA JUMA FARIJALA JUMA CHINANGALI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA Tsh. 17,714,000.**

Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 30/12 mwaka2020 **saa 2:30** asubuhi kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Na kama haukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itadhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 21/12/2020.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**MOSES R MSYETA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj aina ya TVS king yenye namba za usajili **MC 728 CAS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

**Taarifa ya polisi**
**MBE/MBE/RB/877189/2020.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**
**SHERIA YAUSAJILI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO PAMOJA NA STAKABADHI ZA MALIPO YA KIWANJA**

Barua ya toleo (letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kiwanja
(New offer charges & land Rent receipt ). Kiwanja Na .101 kitalu 'Y' Mwakibete ,jiji la Mbeya
Mmiliki aliyeandikishwa :RUKIA HAMZA TAGALILE wa S.L.P. 821 Mbeya
Waombaji MOHAMEDALLY SHABANI na RAMADHAN ALLY SHABANI wa S.L.P 187 RUKWA
Ardhi: kiwanja na. 101 kitalu ' Y' MWAKIBETE , JIJI LA MBEYA
Taarifa imetolewa kwamba barua ya toleo (letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipoya kodi ya kiwanja ya kumiliki ardhi (New offer charges & Land Rent receipts) vilivyotajwa hapo juu vimepotea na ninakusudiakutoa nakala halisi ya Barua ya Toleo (letter of offer ) ya kiwanja pamoja na stakabadhi zote za malipoya kodi ya kiwanja badala yake iwapohakuna kipingamizi chochote kitakachojitokezandani ya muda ya mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii.
Baruaya toleo (letter of offer)yakiwanja pamojana stakabadhi za malipo ya kodiya kiwanja (new offer and land rent receipt ) halisi vikionekana virudishwe Halmashauri ya jiji la Mbeya S.L.P 149 Mbeya

**Imetolewa na,**

**Jacob M.Ngowi**
**AFISA MTEULE**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

---

## NKAYA COMPANY LIMITED

### MARUDIO YA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **BANK OF AFRICA,** Mdaiwa afuatae anatakiwa alipe deni lake lote ndani ya siku kumi na nne kutokea tarehe ya kutoka kwa hili tangazo. Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kuuzwa kwa mali zake alizoziweka kama dhamana.

| JINA LA MDAIWA | MAELEZO KUHUSU DHAMANA | USAJILI WA DHAMANA | TAREHE & MUDA |
|---|---|---|---|
| GOZA FOOD & PACKAGING | NYUMBA ZA KUISHI | C.T NO.134047 & 134061, LO NO.483729, KIWANJA NAMBA 3003 & 3004, KITALU 'B'. MALI INAYO MILIKIWA NA NDUGU ZAMDA AMRAN MDEMU ILIYOPO PUGU MWAKANGA MANISPAA YA ILALA | 05/1/2021 Saa 04:00 asubuhi |
| GOZA FOOD & PACKAGING | NYUMBA YA KUISHI | LESENI YA MAKAZI KND/TNDFKC11/78 PAKACHA, KATA YA TANDALE MANISPAA YA KINONDONI MALI INAYOMILIKIWA NA NDUGU GODFREY ZACHARIA NSERERE | 05/1/2021 Saa 04:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na asilimia 75% atatakiwa kumaliza ndani ya siku kumi na nne endapo atashindwa kulipa kwa muda huo uliowekwa ,pesa aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.
2. Ukaguzi wa mnada utafanyika siku ya mnada.
3. Gharama za kuhamisha mali au kumtoa mtu ndani pamoja na kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.
4. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
5. Endapo yeyote atajitokeza kuharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kulazimika kulipa gharama za mnada.
6. Dalali wa mnada ni Nkaya Company Limited ndio wenye mamlaka na maamuzi ya mwisho ya kumtangaza mshindi.

**MAWASILIANO NKAYA: 0753 000 825/ 0626 180 070**


***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Polisi yadaiwa kumkamata mwanaharakati Opiyo

**Kampala, UGANDA**

POLISI nchini Uganda imemkamata mwanaharakati wa kutetea haki za binadamu, Nicholas Opiyo ambaye ni mkosoaji wa serikali.

Hata hivyo polisi wamewaruhusu mawakili wa mwanaharakati huyo maarufu, kuzungumza naye.

Hiyo ni baada ya muda wa saa 18 tangu kukamatwa kwake juzi, huku wanaharakati wakikosoa kuwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Ijapokuwa awali, polisi walikanusha kumkamata, baadaye walikubali kwamba wanamshikilia kwa tuhuma za uhalifu wa kutakatisha fedha.

Kulingana na wanaharakati wa haki za binadamu pamoja na jumuiya ya wanasheria, kukamatwa kwa Opiyo hakujawashangaza sana.

Wanaelezea kuwa sababu za kumkamata ni za kisiasa zinazolenga kuvunja moyo na ari ya kufuatilia mchakato wa uchaguzi, pia azma yake ya kuchunguza vyanzo vya vifo vya watu 54 mwezi uliopita.

Wanasema kuwa mchakato wote wa kumkamata ni kuwafedhehesha wanasheria kwa kuwa, alitekwa nyara na maofisa waliovalia nguo za kiraia katika mtaa wa Kamwokya na kumlazimisha kuingia katika gari lisilo rasmi la serikali.

Baada ya Opiyo kukamatwa, habari hizo zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii ikidaiwa kuwa ametekwa nyara na watu wasiojulikana.

Awali polisi ilikanusha kuwa wao ndiyo wamemkamata na pia kudai kuwa hawajui aliko.

Lakini saa mbili usiku, polisi ilithibitisha kukamatwa kwake na kuelezea kuwa ni kuhusiana na uhalifu wa utakatishaji fedha na vitendo vya uchochezi.

Baada ya polisi kuthibitisha kuwa Opiyo alikuwa amezuiliwa katika kitengo cha uchunguzi maalum SIU, wanaharakati, mawakili na jamaa zake waliofika kituo hicho, walizuiwa kumwona.

Hatimaye baada ya saa mbili za mabishano kwenye lango la kituo hicho, mawakili wake akiwamo rais wa jumuiya ya wanasheria, Pheona Wall Nabasa wamekubaliwa kuingia kumwona.

Kulingana na wanaharakati hatua hiyo, ilitokana na shinikizo la kimataifa kwa serikali ya Uganda.

Awali, balozi wa Marekani nchini Uganda, alitoa taarifa ya kukosoa kukamatwa kwa mwanaharakati huyo ikiitaka serikali kuhakikisha usalama wake.

Opiyo ni mshindi wa tuzo ya Ujerumani kwa mpigania haki za binadamu barani Afrika, aliikosoa serikali wiki mbili zilizopita kwa kuzifungia akaunti za mashirika kadhaa yasiyo ya serikali, yaliyokuwa yakijiandaa kutoa elimu ya kiraia kuhusu ushiriki wao katika uchaguzi.

***DW***




Malori yakiwa kwenye foleni katika mpaka wa Dover, kufuatia marufuku ya safari iliyowekwa dhidi ya Uingereza ikiwa ni juhudi za kukabiliana na kuenea kwa kirusi kipya cha corona, wakati maofisa wa WHO wakitazamiwa kulijadili suala hilo, tayari mataifa kadhaa ya Ulaya yamelegeza masharti. **PICHA/DW**

# Abiy aanzisha operesheni mpya dhidi ya magaidi

**Addis Ababa, ETHIOPIA**

WAKATI Jeshi la Ethiopia limekuwa likipambana na chama kilichoasi cha TPLF Jimbo la Tigray kwa zaidi ya mwezi mmoja na nusu, pia Jeshi la Ethiopia linakabiliana na Jeshi la Sudan kwenye mpaka wa nchi hizo mbili.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, aliamua kuanzisha operesheni mpya ya kijeshi katika Jimbo la Benishandul Gumuz, Magharibi mwa nchi.

Lengo likiwa kuyatimua makundi ya kigaidi, ingawa operesheni hiyo imezua hofu ya kutokea kwa vita kati ya Ethiopia na Sudan.

Benishandul Gumuz, jimbo lenye wakazi zaidi ya milioni moja kutoka makabila tofauti, limeendelea kushuhudia visa vingi vya unyanyasaji na mauaji katika miezi ya hivi karibuni.

Jamii ya walio wachache ya Amhara wanaoishi katika mkoa huo ni miongoni mwa makabila yanayolengwa na mauaji hayo.

Serikali ya Addis Ababa, inashtumu makundi mawili, TPLF na Oromo (OLF) kuchochea machafuko ambayo yamechochewa na makundi anayosema ni ya kigaidi.

Mapema wiki hii, Abiy alizuru Jimbo la Benishandul Gumuz na kutangaza mkakati maalum wa kudhibiti jimbo hilo bila kutoa maelezo zaidi.

Waziri mkuu huyo, alikuwa ameandamana na mkuu wa jeshi, na kampeni za nyumba kwa nyumba tayari zimeanza.

Inahofiwa kwamba operesheni hiyo itakuwa na mwelekeo mkubwa wa kikabila kwa kuzingatia mizozo iliyopo kati ya jamii.

Ikumbukwe kwamba jimbo hili ni la kimkakati kwa Addis Ababa kwa sababu huko ndiko kuna bwawa kubwa kwenye Mto Nile, ambalo ni bwawa kubwa zaidi barani Afrika.

***RFI***

# Maandamano makali yashuhudiwa Armenia

**Yerevan, ARMENIA**

MAELFU ya waandamanaji juzi, walikusanyika kwenye mji mkuu wa Armenia wa Yerevan, wakiongozwa na upinzani kwenye kampeni ya kushinikiza Waziri Mkuu Nikol Pashinyan, ajiuzulu.

Wanaeleza ajiuzulu kutokana na mkataba wa mwezi Novemba na Azerbaijan, ili kusitisha mapigano.

Waandamanaji hao waliokuwa kwenye bustani kuu mjini humo, walisikika wakisema kuwa Nikol ni msaliti wakati maofisa wa usalama wakishika doria kwenye ofisi za kiongozi huyo zilizoko karibu.

Kundi lingine linasemekana kuingia kwenye majengo ya serikali na kuzua vurugu, huku wengine wakisemekana kufunga barabara kuu.

Kiongozi wa muungano wa upinzani wenye vyama zaidi ya 12, aliapa kuitisha maandamano ya kila siku hadi Pashinyan atakapokubali kukabidhi madaraka, kwa serikali ya mpito itakayoitisha uchaguzi wa bunge, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

Vazgen Manukian, ambaye ameidhinishwa na muungano huo kwa jina National Salvation Movement, kuongoza serikali ya mpito, aliomba Jeshi la Armenia pamoja na polisi kukaidi amri za Pashinyan na kujiunga na watu wengine.

Awali Pashinyan aliweka wazi kuwa hakuwa na nia ya kuondoka madarakani.

***VOA***

# Serikali ya Kosovo yavunjwa kwa kura moja

**Kosovo, PRISTINA**

KURA moja ya mbunge, imesababisha serikali ya nchini Kosovo, kuvunjwa.

Serikali ya Avdullah Hoti, iliundwa, Juni, imevunjwa baada ya kupoteza kura ya imani iliyopigwa bungeni.

Kufuatia hali hiyo, uchaguzi utarudiwa tena nchini humo.

Kura ya moja ya mbunge ambayo haikuhesabiwa kutokana na hukumu yake ya kifungo cha miezi 15 gerezani, ilisababisha kukosa kura ya imani kwa ajili ya kuunda serikali.

Kwa uamuzi huo wa Mahakama ya Katiba, serikali iliyokuwa imeundwa Juni kwa ushindi wa tofauti wa kura moja katika kura ya imani bungeni, ililazimika kuvunjwa.

Uchaguzi unatarajiwa kuandaliwa tena nchini humo, ndani ya siku 40.

Kufuatia kujiuzulu kwa rais wa zamani wa Kosovo, Hashim Thaji, mnamo Novemba 5 mwaka huu, Spika wa Bunge, Vjosa Osmani, alikabidhiwa jukumu la kuhudumu kama rais.

Osmani, atakutana na viongozi wa vyama vya siasa kuamua tarehe ya uchaguzi.

***TRT***

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA AJITOSA KUMTETEA ARTETA

**LONDON, England**

PEP Guardiola amemwelezea, Mikel Arteta kama "kocha mwenye uwezo" baada ya timu yake ya Manchester City kuifunga Arsenal 4-1 na kufuzu nusu fainali ya Kombe la EFL.

Arteta aliondoka kwenye nafasi yake ya kocha msaidizi wa Guardiola mwaka mmoja uliopita kuchukua nafasi ya kuinoa Arsenal, lakini amekalia kuti kavu baada ya kuanza vibaya msimu huu, ambapo umewaacha washikabunduki hao katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Kwenye mchezo huo wa Jumanne, mabao ya Riyad Mahrez, Phil Foden na Aymeric Laporte yaliiwezesha City kushinda mechi 18 mfululizo kwenye mashindano hayo baada ya Alexandre Lacazette kusawazisha lile la ufunguzi la Gabriel Jesus.

Nafasi ya Arteta ipo kwenye shaka kubwa baada ya Arsenal kuruhusu mabao manne nyumbani kwenye michuano ya EFL kwa mara ya kwanza tangu walipofungwa 5-0 na Chelsea Novemba, 1998, lakini Guardiola hana shaka na uwezo wa Mhispania mwenzake huyo.

"Nini ninachoweza kusema, kila mmoja anajua kwamba tunahukumiwa na matokeo. Anaweza kujitetea yeye mwenyewe vizuri tu," alisema akiiambia Sky Sports.

"Nimefanya nae kazi, tulikuwa na mafanikio pamoja na yeye. Ni kocha mwenye uwezo. Najua nini atafanya. Ana uwezo wa kubadilisha mambo."

Ushindi huo una maana kwamba, City imekuwa timu ya kwanza kushinda mechi nne mfululizo ugenini dhidi ya Arsenal katika mashindano yote tangu Chelsea kati ya mwaka 1960 na 1965.



# FIFA YAANZISHA ZENGWE JINGINE KWA BLATTER

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (FIFA), limeibua madai ya tuhuma mpya juu ya matumizi mabaya ya ofisi katika sekta ya fedha kwa Rais wa zamani, Sepp Blatter.

FIFA imesema tuhuma hiyo mpya kwa Blatter imejikita katika ujenzi wa nyumba ya kutunzia kumbukumbu (makumbusho) iliyopo jijini Zurich nchini Uswisi, ambayo licha ya fedha ya shirikisho kuhusika bado haimilikiwi na Fifa wenyewe.

Tuhuma hiyo imewagusa pia na baadhi ya waliokuwa maofisa katika uongozi wa Blatter kwenye mpango wa ujenzi wa nyumba hiyo, ingawa rais mwenyewe alitangaza kujiuzulu mwaka 2015 baada ya kukumbwa na kashfa ya rushwa.


Blatter mwenye umri wa miaka 84 mara zote amekuwa akikana kuhusika na matumizi mabaya ya ofisi.

Bodi ya usimamizi ndani ya FIFA imesema uongozi uliopita wa Blatter ulilisababishia shirikisho hilo hasara ya pauni milioni 420 katika ujenzi wa makumbusho hiyo.

Mpango wa makumbusho hiyo ulianza mwaka 2013, miaka miwili kabla ya Blatter kutangaza kumwaga manyanga, ambaye alikuwa rais wa shirikisho hilo kwa muda wa miaka 17.

Katika kujibu tuhuma hizo, mwanasheria wa Blatter, Lorenz Erni amesema malalamiko ya FIFA yana mapungufu na yamejikita upande mmoja.

Blatter hivi sasa anaendelea kutumikia adhabu ya miaka sita kwa kutojihusisha na shughuli zozote za kisoka.



# PIRLO

## ALIA NA MOLARI YA WACHEZAJI JUVENTUS

**TURIN, Italia**

ANDREA Pirlo amekataa kumlaumu, Juan Cuadrado kwa kutolewa nje wakati Juventus ikichezea kichapo kikali kutoka kwa Fiorentina na badala yake alihoji molari ya wachezaji wake kabla ya mchezo huo.


Juve ilikumbana na kipigo chake cha kwanza kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, chini ya Pirlo kwenye mechi yake ya 13 tangu achukue mikoba, na pia kuchapwa mabao hayo 3-0 kilikuwa kipigo kikubwa zaidi walichokipata kwenye dimba lao la nyumbani la Allianz tangu mwaka 2011.

Cuadrado alimchezea faulo Gaetano Castrovilli na alionyeshwa kadi nyekundu ya moja kwa moja katika mchezo wake wa 200 kwa miamba hao wa Turin.

Dusan Vlahovic aliipa bao la kuongoza Fiorentina kabla ya Alex Sandro kujifunga na Martin Caceres akafunga la tatu.

"Kilichotokea kwenye kadi nyekundu sio jambo la kujadili," alisema Pirlo akiiambia Sky Sport Italia. "Matokeo hayakuwa kwa sababu ya ari ya Fiorentina, lakini ni kutokana na sisi kutokuwa na molari.

"Ukiwa kwenye hali kama hiyo, unakutana na matokeo kama haya. Ni mechi za kukaribia sikukuu ya Krismas inaweza kutokea hivyo, kwa sababu mawazo ya wote yapo kwenye likizo. Hatukuwa mchezoni na ndio maana tumepoteza.



# SOLSKJAER:

## POGBA ANACHOTAKA NI MATAJI TU

**MANCHESTER, England**

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amerudia kusema tena hana hofu na mtazamo wa Paul Pogba, ingawa anakubali "malengo" ya kiungo huyo wa Manchester United ni kutaka kucheza kwenye timu inayoshinda mataji.

Tangu amerudi pale Old Trafford kutoka Juventus kwa ada iliyoweka rekodi kwenye usajili wa mwaka 2016, Pogba amekuwa akihusishwa mara kwa mara na mpango wa kuondoka United.

Juventus na Real Madrid zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili nyota huyo, huku mshindi huyo wa Kombe la Dunia amekuwa kwenye wakati mgumu wa kuwa kwenye kiwango chake bora.

Msimu bora zaidi wa Pogba ulikuwa ni ule wa 2018-19 wakati alipofunga mabao 13 na kutoa pasi za mwisho tisa katika mechi 35, na msimu uliopita alifunga mara moja na kutengeneza matatu katika mechi 16.

Msimu huu amefunga bao moja katika mechi 10 - saba kati yao akiwa ameanza na kuendelea kuwa katika msimu mwingine mbaya zaidi na hivyo uvumi unaendelea kuvuma kuhusu majaliwa yake.

Ingawa wakala wake, Mino Raiola alibainisha kwamba, Pogba amefikia mwisho wake pale United, lakini Solskjaer amekataa tena kumshutumu mchezaji huyo.

Alipoulizwa kuhusu nyota huyo wa Ufaransa, alisema ni wakati sasa wa United kushinda mataji ili kuwafanya wachezaji wao kuwa na furaha.

"Mara zote hapa Manchester United kunahitajika kushinda mataji," alisema Solskjaer akiiambia ESPN.

"Na unavyodizi kushinda mataji, wachezaji wengi zaidi watataka kucheza hapa, hivyo jambo pekee kwa sasa ni kushinda mataji."

"Paul amekuwa hapa kwa muda sasa, bila shaka anataka kushinda mataji. Ana mtazamo mzuri sana kwenye mazoezi na kucheza soka."

# KAULI YA KOEMAN YAMKERA ZIDANE

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane amekasirishwa na lawama za Ronald Koeman kuhusu maamuzi ya waamuzi kwa kuipendelea Real Madrid, akisisitiza kamwe hataingia kwenye mjadala huo.

Kocha huyo wa Barcelona, Koeman alisema Jumatatu kwamba alishindwa kuelewa kwanini Eibar walishindwa kupewa penalti wakati wakifungwa 3-1 na Madrid.

Wakati Eibar wakiwa nyuma kwa bao moja, mpira ulionekana kumgonga mkononi mlinzi, Sergio Ramos katika eneo la penalti.


Lakini mwamuzi hakutoa adhabu na wala hakwenda kuangalia kwenye VAR na Koeman alidai kwamba, kikosi hicho kilichomaliza na wachezaji 10 uwanjani kilionewa.

Kauli hiyo ikamwibua Zidane Jumanne ambapo alijibu kwa kusema: "Ni jambo linalokasirisha kwa sababu sijawahi kuwazungumzia waamuzi.

"Nafikiri waamuzi wapo kwenye mchezo na wanafanya kazi nzuri. Kama kila mmoja wetu hao akijaribu kufanya kazi yake vizuri. Sijihusishi nao. Ni kazi ngumu sana ile.

"Kile anachozungumza Koeman siwezi kujikita nacho. Tunachotakiwa ni kuangalia mechi zilizopo mbele yetu."





# SIMEONE AFIKISHA MECHI 300 ZA USHINDI ATLETICO

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amezungumzia mtazamo wake baada ya kufikisha mechi 300 za ushindi akiwa na klabu hiyo na kuelezea ni jambo lenye maana kubwa sana kwake.

Atletico ilionyesha kiwango cha kuvutia Jumanne wakati kikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Real Sociedad pale kwenye dimba la San Sebastian na kupaa kileleni mwa LaLiga kwa pointi tatu zaidi.

Ilikuwa ni mechi yao ya tisa kucheza bila kuruhusu bao kwenye mechi 13 za ligi msimu huu, tangu msimu wa 1995-96 waliporuhusu mabao machache ya kufungwa (manne) katika hatua hii.

Ushindi huo unamaanisha kwamba, Simeone ambaye anakinoa kikosi hicho tangu mwaka 2011, amebakisha mechi nane kufikia rekodi ya kocha Luis Aragones aliyekiongoza kikosi hicho kushinda mechi 308 katika mashindano yote.

Na Simeone akatambua kufikia rekodi hiyo ni jambo la kujivunia zaidi kwake.

"Inamaana kubwa sana kwangu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilikuja kwenye klabu hii nikiwa sina wazo la kuiongoza Atletico kufikia idadi hii ya mechi za ushindi.

"Nawashukuru sana Miguel (Angel Gil, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Atletico) na Enrique (Cerezo, rais wa klabu) kwa kunileta klabuni hapa."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AVUNJA REKODI YA PELE

Ni baada ya nahodha huyo wa Barca kufunga mabao mengi zaidi ya mkongwe huyo wa Brazil...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi alifunga bao lake la 644 wakati Barcelona ikipata ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Real Valladolid na kuvunja rekodi ya Pele ya kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi katika klabu moja.

Mshambuliaji huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 33, alifunga bao la tatu kwa Barcelona kwa kumpiga chenga mlinda mlango, Jordi Masip kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, juzi Jumanne.

Messi aliifikia rekodi ya Pele ya kufunga mabao 643 kwenye mchezo uliopita na kuwa sawa na gwiji wa Brazil mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote ambaye aliichezea Santos kwa miaka 18.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or aliifikia rekodi hiyo kwa kufunga dhidi ya Valencia Jumamosi iliyopita na juzi Jumanne akaipiku rekodi ya Pele. Akiwa ametengeneza bao la ufunguzi lililofungwa na Clement Lenglet na akiwa amefanya kazi ya ziada kwenye bao la pili la Barca dhidi ya Real Valladolid, Messi alifunga la tatu kwa pasi ya mwisho ya Pedri dakika ya 65 na kufanya matokeo kuwa 3-0.

Pamoja na kuvunja rekodi ya Pele, pia Messi alifikisha mabao 451 kwenye Ligi Kuu Hispania maarufu LaLiga.

Jitihada zake Messi kwenye mchezo dhidi ya Valencia zilimfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufikisha mabao 450 kwenye klabu moja katika ligi kubwa tano za Ulaya.

## KWA UFUPI

**GREALISH AGOMBEWA**

LIVERPOOL wamejiunga na Manchester United na Manchester City katika mbio za kuwania saini ya Jack Grealish, mwenye umri wa miaka 25, huku Aston Villa wakitaka dau kubwa zaidi kwa kiungo huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya England. ***(Mirror)***

**ALABA AKARIBIA UNITED**

MANCHESTER United wana matumaini ya kuzipiku timu kama Real Madrid na Barcelona katika kuipata saini ya mlinzi wa Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake kule Bayern Munich unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

**LIVERPOOL, CHELSEA VITANI**

LIVERPOOL na Chelsea nazo zimeingia kwenye mbio moja za kutaka kumsajili, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, mara tu mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu kule Bayern Munich. ***(Sun)***

**KABAK ASHUKA THAMANI**

TIMU za Manchester United na Liverpool ni miongoni mwa klabu kadhaa ambazo tayari zimekwisha onyesha nia yao ya kutaka kumsajili mlinzi wa klabu ya Schalke, Ozan Kabak (20), huku klabu hiyo ya Bundesliga ikishusha bei yake na sasa ikitaka ilipwe pauni milioni 25 badala ya milioni 40 kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Uturuki. ***(Mail)***

**ARSENAL YAMTAKA ERIKSEN**

ARSENAL wanaangalia uwezekano wa kumwania kiungo wa kati wa Inter Milan na Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Gazzetta dello Sport via Sport Witness)***

**TARKOWSI SOKONI**

WEST Ham, Leicester City na klabu nyingine za Ligi Kuu England zinawania kumsajili mlinzi wa Burnley na England, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 29, wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Eurosport)***

**SALAH KUONGEZWA MSHAHARA**

LIVERPOOL wanataka kumwongezea mshahara mshambuliaji wao kutoka Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 28, ili kuzima ndoto za Real Madrid, Barcelona na Paris St-Germain zinazomwania. Salah kwa sasa analipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Goal)***

**LEVERKUSEN, UNITED KUTETA**

KLABU ya Bayer Leverkusen imezungumza na Manchester United juu ya kutaka kumpa mkataba wa kudumu, Brandon Williams mwenye umri wa miaka 20 ambaye anacheza hapo kwa mkopo. ***(Sky Germany via Sky Sports)***

**LEEDS YAMTAKA TRAORE**

KLABU ya Leeds United wanamtaka winga wa Timu ya Taifa ya Hispania, Adama Traore (24), huku kukiwa hakuna uhakika kuhusu majaliwa yake ya baadaye katika klabu yake ya Wolves kutompa muda wa kutosha wa kucheza uwanjani. ***(90 min)***

**RASHFORD ATAJWA BARCA**

MGOMBEA urais wa Barcelona, Jordi Farre, anasema klabu hiyo inahitaji kuimarisha safu yake ya ushambuliaji na amemtaja nyota wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 23, kuwa miongoni mwa wachezaji anaowahusudu. Farre (45), pia ameahidi kumsajili tena Neymar. ***(90 min)***

ARSENAL MAMBO MAGUMU

HABARI MICHEZO

# MSHAMBULIAJI LUPOPO ASAJILIWA RASMI AZAM

**Na Saada Akida**

BAADA ya uongozi wa Azam FC kufanikiwa kumsajili mshambuliaji wa FC Lupopo, Mpiana Moziz, sasa mabosi wa klabu hiyo wako katika mchakato wa kusaka kipa mpya kutoka nje ya nchini kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema baada ya Mpiana amesaini mkataba wa mwaka mmoja na wanaamini ataisaidia timu yao kupata matokeo mazuri.

Popat alisema baada ya kumaliza mechi dhidi ya Ruvu Shooting, walikutana na Kocha Mkuu, George Lwandamina ambaye alipendekeza kusajiliwa kwa Mpiana pamoja na kipa mwingine.

Alisema tayari wameanza kufanyia kazi mapendekezo hayo ya Lwandamina ili kurejesha makali ya kikosi chao.

"Katika mechi zetu tano za mwisho hatukufanya vizuri, tukianzia mchezo dhidi ya Yanga tumefungwa, pia kuambulia pointi nne katika mechi nne, huku mbili tukicheza ugenini na mbili tukilazimishwa sare nyumbani."

"Tumegundua shida ya timu yetu, baada ya kuondoka kwa Thiery Akono ambaye tumemuuza kwenda nchini Malaysia kwenye Klabu ya Negeri Sembilan, tumemleta Mpiana, sasa kocha anahitaji kipa kutoka nje, hilo linafanyiwa kazi," alisema Popat.

Wakati huo huo, taarifa za uhakika zilizofikia gazeti hili zinasema Azam FC inaendelea na mchakato wa kusajili mlinda mlango kutoka nje ya Tanzania, lakini ikilazimika kumwacha nyota mmoja wa kigeni ili kufikia idadi ya wachezaji 10 wanaoruhusiwa kwa mujibu wa kanuni.

Nyota wa kigeni walioko katika kikosi cha Azam ni pamoja na Daniel Amoah, Obrey Chirwa, Prince Dube, Ally Niyonzima, Nicholas Wadada, Bruce Kangwa, Richard Dijdo, Never Tegere, Yakubu Mohammed na Mpiana.

Mpiana amesajiliwa baada ya kufuzu vipimo vya afya na utimamu wa mwili na taratibu za vibali zitakapokamilika ataanza kuitumikia timu hiyo kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA na Kombe la Mapinduzi.




Mshambuliaji mpya wa Azam FC, Mpiana Moziz (kulia), kutoka FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DR-Congo) akiwasili nchini juzi. Mpiana tayari ameshasaini mkataba wa mwaka mmoja. **PICHA: MTANDAO**

## Rekodi mpinzani wa Class zinatisha

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA wa Tanzania, Ibrahim Class anatakiwa kufanya kazi ya ziada kwa ajili ya kuhakikisha anafanya vyema dhidi ya mpinzani wake kutoka Malawi, Dennis Mwale kutokana na rekodi zake kuwa za juu.

Class anatarajiwa kumkaribisha Mwale katika pambano la uzito mwepesi linalotambuliwa na Shirikisho la Ngumi la Kimataifa la WBF litakalofanyika Januari 29, mwakani kwenye ukumbi wa Next Door Arena.

Pambano hilo limeandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sports chini ya Mwasisi na Ofisa Mtendaji Mkuu, Kelvin Twissa na kudhaminiwa na Aza.

Rekodi zinaonyesha tangu bondia huyo ameanza kupigana mwaka 2017, amefanikiwa kushinda mapambano nane ambapo kati ya hayo, matatu ameshinda kwa TKO na matano ameshinda kwa pointi.



Rekodi zinaonyesha mabondia waliopigwa kwa TKO na Mwale hawajavuka raundi ya tano ambapo pambano la mwisho kushinda kwa staili hiyo ya ushindi ilikuwa Agosti 31, mwaka jana dhidi ya Khaya Busakwe katika pambano lililofanyika kwenye Ukumbi wa Turfonyein Rase Course jijini Johannesburg, Afrika Kusini.

Mbali ya pambano hilo, siku hiyo kutakuwa na mapambano mengine makali ya utangulizi ambapo bondia wa kike Mtanzania, Stumai Muki, atazichapa na Revai Madondo wa Zimbabwe katika uzito wa fly wa raundi sita wakati Mkenya Rayton Okwiri atapambana na Jimmy Mabundji wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, huku Shaaban Jongo atazipiga na Shawn Miller raia wa Marekani katika uzito wa Cruiserweight la raundi 10.

Pia kutakuwa na pambano kali kati ya bondia Nasibu Ramadhan dhidi ya Nkosinathi Biyana wa Afrika Kusini katika uzito wa feather raundi 10.

## Panga lanukia Dodoma Jiji FC

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Dodoma Jiji FC umesema tayari umepokea ripoti ya kiufundi kutoka kwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbwana Makata yenye tathmini ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji, Fortunatus Johnson, alisema baada ya kupokea ripoti hiyo, Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo inatarajia kukutana leo kwa lengo la kuijadili na kuifanyia kazi.

Johnson alisema katika ripoti hiyo watajua madhaifu ya kikosi chao, nyota wanaoachwa, watakaotolewa kwa mkopo pamoja na wachezaji wapya waliopendekezwa kusajiliwa kwenye kipindi cha dirisha dogo.

"Tayari ripoti nimeshakabidhiwa ila Kamati ya Utendaji hatujapata muda wa kukaa, kesho (leo), jioni tutakaporudi Dodoma kutakutana na kuipitia na kuona madhaifu yetu, tutajua wachezaji wapi ambao tutawaongeza kipindi hichi cha dirisha dogo," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza wanatarajia Ijumaa wataweka wazi majina ya wachezaji wanaotemwa na ingizo jipya watasajiliwa kwa ajili ya kuongeza nguvu ndani ya kikosi cha timu hiyo.

"Huu ni muda wa kufanyia kazi upungufu wa kikosi, ligi ni ngumu sana na kipindi cha usajili tutahakikisha tunaleta wachezaji ambao watatusaidia katika mechi zetu za mzunguko wa pili," aliongeza.

## JKT yazichunia Simba, Yanga

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuhitaji kuimarisha kikosi chake, uongozi wa JKT Tanzania umesema hauna mpango wa kusajili wachezaji kutoka katika klabu kongwe hapa nchini za Simba na Yanga katika kipindi cha dirisha dogo ambalo limeshafunguliwa.

Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Abdul Nyumba, alisema timu yake haitasajili nyota yoyote kwa mkopo kutoka timu hizo na badala yake itaangalia wachezaji waliong'ara kwenye klabu za madaraja ya chini.

Nyumba alisema tayari wamepokea mapendekezo ya kusajili wachezaji katika nafasi tatu ikiwamo beki wa kati, beki wa pembeni pamoja na mshambuliaji na utekelezaji wa kusaka nyota hao umeshaanza.


Aliongeza watahakikisha wanapita katika matakwa ya mapendekezo waliyopewa na Kocha Mkuu wa timu yao, Mohammed Abdallah 'Bares' kwa ajili ya kuimarisha kikosi cha timu hiyo na si vinginevyo.

JKT Tanzania inashika nafasi ya 15 ikiwa imeshinda michezo mitatu, sare tano na kupoteza mechi nane baada ya kushuka dimbani mara 16.

# Michezo

Alhamisi Desemba 24, 2020

Nipashe

MESSI AVUNJA REKODI YA PELE

HABARI UK 22

# SIMBA YAJIWEKA MTEGONI AFRIKA

## ●●●Yapoteza ugenini Zimbabwe kwa bao 1-0, huku Namungo ikitakata...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba wamekubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa FC Platinum katika mechi ya kwanza ya hatua ya kwanza iliyochezwa mjini Harare, Zimbabwe jana.

Kosa lililofanywa na beki wa kati ya Simba, Paschal Wawa kushindwa kuokoa mpira na kumzuia straika machachari wa Platinum, Perfect Chikwende, lilimfanya mchezaji huyo kumtoka kwa kasi na kupiga shuti kali lililojaa wavuni baada ya kumshinda kipa wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Aishi Manula kudaka dakika ya 17.

Kwa matokeo hayo, Simba italazimika kupata ushindi wa kuanzia mabao 2-0 katika mechi ya marudiano itakayochezwa Januari 6, mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam ili isonge mbele kwenye michuano hiyo.

Mechi ilianza kwa timu kucheza zaidi katikati ya uwanja badala ya mashambulizi, kila timu ikionekana kusoma mchezo wa mwenzake.

Nusura Simba isawazishe dakika mbili baadaye, baada ya Luis Miquissone kupiga shuti kali lililotoka pembeni kidogo mwa lango, kufuatia krosi iliyopigwa na Hassan Dilunga.

Miquissone aliikosesha Simba bao dakika ya 39, baada ya kuambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto, lakini alikuwa mchoyo, badala ya kuwapa wenzake, Clatous Chama na Meddie Kagere waliokuwa ndani ya eneo la hatari kwa kupiga shuti ambalo liliambaa mbele ya lango na kutoka nje.

Kagere alishindwa kuunganisha mpira wa kichwa dakika ya 39, baada ya krosi iliyochongwa kwenye wingi ya kulia na Dilunga na kuifanya Simba ipoteze nafasi nyingine ya kupata bao la kusawazisha katika mchezo huo.

Kipindi cha pili, Simba iliwatoa Kagere, Erasto Nyoni na Hassan Dilunga na nafasi zao kuchukuliwa na Miraji Athumani, Mzamiru Yassin na Rally Bwalya.

Kuingia kwa Bwalya kwa kiasi kikubwa kuliibadilisha Simba ambayo baadhi ya wachezaji wake tegemeo hawakuwa kwenye kiwango bora kama Chama, Miquissone na Kagere.

Baada ya Bwalya kuingia, alisababisha FC Platinum warudi nyuma na kuanza kucheza kwa kuzuia na kushambulia kwa kushtukiza tofauti na walivyocheza dakika 45 za kwanza.

Dakika chache baada ya kipindi cha pili, Manula aliokoa kombora kali la juu lililopigwa na Gift Mbweti na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Dakika ya 68, Bwalya alibaki yeye na kipa Petros Mhari ambaye alipangua shuti lake na kuwa kona ambayo nusura izae bao kama kichwa na Joash Onyango kisingetoka nje kidogo ya lango, huku Simba ilifanikiwa kuukwamisha mpira wavuni kupitia kwa Mugalu, lakini mwamuzi msaidizi alikataa kwa madai mfungaji alikuwa ameotea ikiwa ni dakika ya 75.

Dakika za mwisho Simba ilikosa mabao mawili ya wazi, moja likikoswa na Chama aliyepiga shuti lililowababatiza mabeki wa FC Platinum na Mugalu ambaye alipiga kichwa cha kudundisha, lakini mpira ukapaa langoni kwenye dakika za nyongeza.

Katika mchezo huo, Simba ilimkosa nahodha wake, John Bocco anayeongoza kwa kupachika mabao kwenye Ligi Kuu Bara huku wapinzani wao wakifanikiwa kuwabana Chama na Miquissone na hivyo kuwafanya washindwe kuonyesha makali yao.

Wakati huo huo wawakilishi wengine wa Tanzania Bara, Namungo wameendelea kufanya vyema katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kuwafunga wapinzani wao, El Hilal Elobied ya Sudan mabao 2-0 katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

Mabao ya Namungo inayofundishwa na Mzanzibar Hemed Suleiman 'Morocco' katika mechi hiyo yalifungwa na Sixtus Isabilo dakika ya 13 na Steven Sey akifunga la pili dakika ya 30.



Mshambuliaji wa Yanga, Saido Ntibazonkiza (kulia), akimtoka mchezaji wa Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya jana. Yanga ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## YANGA HABARI NYINGINE BARA

**Na Adam Fungamwango**

YANGA imeendelea kujiimarisha kileleni baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya Ihefu FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya.

Kwa ushindi huo, Yanga imefikisha pointi 43 na kuweka rekodi ya kuwa timu pekee iliyomaliza mzunguko wa kwanza bila kufungwa mechi hata moja, huku wenyeji Ihefu wakisalia na pointi 13.

Shambulio la kwanza Yanga kwenye lango la Ihefu lilizaa goli, baada ya kiungo chake mpya iliyomsajili katika kipindi cha dirisha dogo, Saido Ntibazonkiza alipowalamba chenga mabeki kadhaa wa Ihefu na kumegea pasi safi, Deus Kaseke aliyeuweka wavuni dakika ya 12 ya mchezo huo.

Lilikuwa ni bao la nne kwa Kaseke msimu huu wa 2020/21 ambao unaonekana kuwa mzuri kwa winga huo.

Dakika ya 50, Yacouba Songne, aliifungia Yanga bao la pili wakati Feisal Salum alimalizia karamu hiyo ya magoli kwa kufunga goli la tatu dakika ya 60.

Golikipa, Deogratius Munishi 'Dida' ambaye alisajiliwa na Ihefu kipindi cha dirisha dogo ndiye aliyekuwa shujaa kutokana na kuiokoa timu hiyo kufungwa mabao mengi kipindi cha kwanza ambapo dakika ya 21 na 32 alizuia mashambulizi makali ya wachezaji wa Yanga, yakiongozwa na Yacouba.

Mapema tu dakika ya nane, Ihefu ilikosa bao la wazi, baada ya Juma Mahadhi kupiga shuti kali lililotemwa na kipa, Metacha Mnata na kumkuta nahodha wa timu hiyo Joseph Kinyozi ambaye badala ya kuuweka mpira wavuni, alimpasia mikononi kipa Metacha ambaye alikuwa amelala chini.

Katika mechi ya mapema jana iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma wenyeji JKT Tanzania ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC FC kutoka jijini, Dar es Salaam.

Shukrani kwa mshambuliaji, Danny Lyanga ambaye alifunga mabao yote mawili katika mchezo huo na kuifanya timu yake ifikishe pointi 17, lakini ikibakia kwenye nafasi ya 15 katika msimamo wa ligi hiyo.


9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042